**KESI** kina Mdee yakwama kortini, vigogo CHADEMA waitwa Korti Kuu

UKURASA 4



**TRA** yatangaza ongezeko tozo malipo kodi ya majengo kupitia mita za Luku

UKURASA 5


ama
ALHAMISI JULAI 27, 2023
AFYA NA MAZINGIRA
Ni maajabu ya papai kwako, kama huli, anza sasa hivi
Wabunifu UDSM wanapokonga wapishi jikoni, wawaletea 'jikosola'
Ndiyo ujumbe wa wakulima, wazalishaji mbegu kwa SMZ
•Washangaa mchakato wa sheria unachelewa, wataka ulinzi Vs GMO
Inaendelea Uk. 1

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581384

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Ukimya nyongeza ya mishahara wang'ata

**TUCTA** yasema wafanyakazi hawajaona 'jambo lao', serikali yaahidi... *Endelea Ukurasa wa 3*



Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya

## Ruto akubali kukutana na Odinga

UKURASA 19



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Kenya, William Ruto, kando ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu rasilimali watu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

KASI YA KUZAANA

## SAMIA AIPA AFRIKA ANGALIZO ONGEZEKO VIJANA BILA AJIRA

UKURASA 2

**MICHEZO** **ROBERTINHO: SIMBA NI KUBWA HAIOGOPI TIMU AFRIKA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Samia aipa Afrika angalizo ongezeko la vijana

**Na Romana Mallya**



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na marais mbalimbali waliohudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Rasilimali Watu jijini Dar es Salaam jana. Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, Rais wa Madagascar, Andry Nirina Rajoelina, Rais wa São Tomé na Principe, Carlos Vila Nova, Rais wa Kenya, William Ruto na Rais wa Malawi, Lazarus McCarthy Chakwera. **PICHA: IKULU**

AFRIKA sasa ina zaidi ya watu bilioni 1.4 idadi ambayo ikitumika vyema inaweza kuwa kwa maendeleo lakini inaweza kuwa mzigo iwapo itatumika vibaya kutokana na kuongezeka bila kuendana na hali ya uchumi.

Rais Samia Suluhu Hassan, mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu rasilimali watu, alisema hayo katika hotuba yake jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano uliohudhuriwa na viongozi 43 kutoka nchi za Afrika.

Miongoni mwa viongozi walioshiriki mkutano huo ni marais kutoka Kenya, Madagascar, Malawi, Sao Tome and Principle, Sierra Leone na Mozambique, Makamu wa Rais kutoka Benin, Uganda, Sudan Kusini na Zambia, Mawaziri Wakuu wa Burundi, Eswatini na Somalia, Naibu Mawaziri Wakuu wa Cape Verde na Somalia.

"Ni lazima tuwafundishe watoto wetu kuhusu uzazi wa mpango. Kama nilivyosema Afrika ina idadi kubwa ya watu inaweza kutuletea tija au ikatuletea mambo yasiyofaa. Mkutano huu unafanyika wakati mwafaka hasa ikizingatiwa kwa sasa Afrika ndilo bara lenye vijana wengi zaidi. Takwimu zinaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2050 Afrika itatoa nchi 10 zenye idadi kubwa zaidi ya vijana duniani," alisema.

Kwa mujibu wa Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF), alisema zaidi ya asilimia 60 ya watu ndani ya Afrika ni vijana walio chini ya miaka 25 na inadakidiriwa ifikapo mwaka 2030, Afrika itakuwa na asilimia 42 ya vijana wote duniani.

"Jambo la pili, idadi kubwa ya vijana tuliyo nayo ni fursa pekee kwa mageuzi ya kiuchumi. Badala ya kuacha vijana hawa wavuke bahari wapigwe njiani na kuzamishwa kwamba wanakwenda Ulaya kutafuta maisha bora, tuwaendeleze ili maisha bora wayapate hapa hapa Afrika," alisema.

Jambo lingine alilitaja kuwa ni kuongeza manufaa yanayotokana na elimu na mafunzo yanayotolewa katika nchi mbalimbali ili kuwapa uwezo vijana kuongeza tija na kujenga uchumi.

Kwa mujibu wa Samia, jambo la nne ni kuongeza uwekezaji katika sekta zingine zinazoleta ufanisi katika huduma za elimu na afya kwa kuwekeza katika miundombinu, kuongeza huduma za usafiri, nishati, umeme, maji na usafi wa mazingira huku akibainisha kuwa jambo la tano ni utekelezaji wa programu za hifadhi ya jamii katika uzalishaji.

Alisema katika kutumia fursa kufungua rasilimali watu Afrika, ni wajibu wa kimaadili na ni sharti muhimu la kiuchumi kuongeza nishati kwa jamii na rasilimali fedha kwenye elimu na maendeleo ya rasilimali watu kuijenga Afrika yenye mafanikio jumuishi.

"Kwa hivyo, inatupasa tuunganishe nguvu za serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi ili kufanya uwekezaji unaohitajika na kujenga mazingira wezeshi ya kukua na kuendelea kwa rasilimali hii muhimu ambayo ni watu wetu, vijana wetu. Kwa pamoja tunaweza kujenga mustakabali wa Afrika kwa kuhakikisha ndoto za vijana wetu zinatimia," alisema.

Pia alisema suala la maendeleo ya rasilimali watu haliwezi kuja kwa kubahatisha na halina mbadala, hivyo lazima kuwe na mipango madhubuti katika kuiendeleza kwa manufaa ya Afrika.

**KUHUSU MKUTANO**

Kuhusu mkutano huo, Rais Samia alisema ndio utakaoamua uwekezaji unaohitajika ili kuleta tija na kuchochea maendeleo ya Afrika huku akisisitiza hakuna muda wa kujadili hilo zaidi ya sasa.

Alisema zaidi ya muongo mmoja sasa, Afrika imepitia ukuaji na uimarikaji mkubwa wa uchumi katika sekta tofauti na kuifanya kuja na misamiati kadhaa ili kuikwamua kutoka kwenye utegemezi.

"Pia kulifanyika jitihada za makusudi kuhakikisha Afrika inajenga uchumi wake kwa kutumia rasilimali ilizo nazo kujiletea maendeleo na kwamba maendeleo hayo yameonekana lakini kwa baadhi ya nchi hayakuonekana au kuonekana kwa kiasi kidogo.

**MALENGO SABA**

Rais Samia alisema Afrika inahitaji mageuzi makubwa katika nyanja zote muhimu za uzalishaji na maendeleo.

"Haya ndio malengo na madhumuni ya maendeleo ya Afrika tunayoitaka ya mwaka 2063 ambayo imejiwekea malengo saba. Hapa ninajielekeza kuyazungumzia malengo manne. Moja, Afrika ambayo mafanikio yake yanajikita kwenye ukuaji jumuishi wa uchumi na maendeleo endelevu.

"Pili, Afrika yenye utangamano kisiasa kwa kuzingatia fikra za majumui na mwekeleo wa kimapinduzi, tatu, Afrika inayozingatia misingi ya utawala bora, demokrasia haki za binadamu na utawala wa sheria," alisema.

Alilitaja lengo la nne ni kuwa na Afrika ambayo maendeleo yake yanatokana na watu wa kutumia vipaji vyao hususan wanawake na vijana na kutoa makuzi bora kwa watoto, jambo ambalo alisema ndilo lililowakutanisha kwenye mkutano huo.

**VIONGOZI WENYE MAONO**

Rais Samia alisema majibu ya masuala hayo pia, yatatoa mwelekeo wa serikali zao kwa viongozi wenye maono, kujenga sera kwenye maendeleo ya watu na kufuatiwa na maendeleo ya vitu.

Alinukuu maeneo ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliyowahi kusema alipohutubia mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN, New York kuwa: "Maendeleo ni watu, watu ndio walengwa, ndio waanzilishi na wanufaika wa chochote kinachohusu maendeleo."

Rais Samia alisema kwa mantiki hiyo, hawawezi kuikomboa Afrika kama hawataelekeza nguvu kwenye maendeleo ya rasilimali watu kwa kuwapa maarifa na ujuzi unaohitajika katika kuyatumia na kubadilisha mazingira kwa manufaa.

Alisema wanapozungumzia uwekezaji wa rasilimali watu, huanza tangu mtoto anapozaliwa kwa maana ya upatikanaji wa lishe bora na chanjo stahiki ili kuondoa udumavu ambao hupunguza ugonjwa wa kuelewa na uwezo wa kusoma vizuri.

Ili kuweka msingi mzuri wa elimu, wanapaswa kuwa na maandalizi ya elimu hasa ya awali kwa ajili ya kuwaandaa watoto kimwili, kiakili, kijinsia na kiubunifu na ili elimu itoe matokeo chanya, ni lazima kuwa na mitaala yenye kukidhi matakwa ya soko la ajira.

Rais Samia alinukuu kauli ya mwasisi wa taifa huru la Afrika Kusini, Nelson Mandela, aliyewahi kusema: "Elimu ndiyo silaha yenye nguvu zaidi inayoweza kutumika kubadilisha ulimwengu."

**MAKAMU WA RAIS WB**

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia (WB) anayesimamia Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa, alisema Afrika inakabiliwa na changamoto za rasilimali watu hata kabla ya UVIKO - 19 na kwamba vijana wana mchango wa asilimia 14 tu.

Alisema kusini mwa Jangwa la Sahara, changamoto ni uwezo mdogo wa kujifunza kutokana na watoto wa umri wa miaka 10 kushindwa kusoma na kuandika, hivyo elimu pekee ndiyo kitovu cha maendeleo kwa Afrika.

Kwakwa alisema kwenye masuala ya uongozi, Tanzania imepata mafanikio makubwa kuhakikisha watoto wote hasa wasichana waliojifungua wanaendelea na masomo na Kenya imeboresha katika kuandaa mtaala na usimamizi wa walimu. Alisema Jamhuri ya Kidemokrsasi ya Congo imetenga fedha zaidi kwenye elimu na Zambia kutumia mifuko ya hifadhi kukabiliana na bei za vyakula kwa kuanzisha mifumo ya kidigitali.

"Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zinahitaji kuwekeza zaidi kwenye elimu. Suala la fedha si changamoto pekee, hivyo tunahitaji kuimarisha ufanisi wa elimu. Tunatakiwa kuimarisha mishahara ya walimu, kuwapa tuzo, motisha ili kuendeleza elimu.

"Zaidi ya asilimia 50 ya walimu hawafundishi kwa ufanisi, hili si jambo jema, tunatakiwa kuwa na usambazaji wa walimu maeneo yote. Iko haja ya kuimarisha stadi za kazi kwa walimu na tunahitaji kupata fedha zaidi ili kufikia malengo ya kimataifa," alisema.

**VIJANA WA KIKE**

Makamu wa Rais Uganda, Jessica Alupo, alisema katika nchi yake wanawawezesha vijana wa kike kwa kutoa kipaumbele na wanawake wanashiriki maudhurio ya kliniki na elimu ya wasichana imewekewa mkazo.

"Tumeanzisha sera tunahamasisha maslahi ya wasichana kuwa viongozi kuanzia udiwani ngazi ya wilaya. Katika Bunge, mfano viti maalum, mimi nimeteuliwa kupitia viti maalum. Rais anaweka suala la wasichana kama la kipaumbele, WaziriMkuu ni mwanamke, Spika wa Bunge ni mwanamke," alisema.

Makamu wa Rais wa Zambia, Mutale Nalumango, alisema kuhusu vijana wanapaswa kujua ni aina gani na kundi lipi la vijana wanaowalenga.


## TANGAZO



Jina- **GILBERT KAIZILEGE RWIZA**

Mtu aliyetajwa hapo juu (Pichani) si mwajiliwa tena wa Lake Cement Limited. Umma na mheshimiwa mteja wa **Lake Cement Ltd** waonywa na kuonywa kutojihusisha naye katika jambo lolote linalohusiana na aina ya biashara ya Lake Cement Ltd.

Kwa kosa lolote la yeye kutumia aina yoyote ya hati za kampuni mali ambayo aliimiliki wakati wa ajira yake, Lake Cement haitawajibika kwa hilo. Tunawakatisha tamaa wanajamii wasiwe na mahusiano naye zaidi.

**Imetolewa na Lake Cement Limited**

# Ukimya nyongeza mishahara wang'ata

Na Halfani Chusi

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limeiomba serikali kutimiza ahadi yake ya nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan katika Sikukuu ya Wafanyakazi mwaka huu.

Mkoani Dar es Salaam jana, Rais wa TUCTA, Tumain Nyamhokya, aliikumbusha serikali kutimiza ahadi hiyo ili kuongeza morali kwa wafanyakazi katika kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema kuwa katika kipindi cha miezi takribani mitatu, wameona serikali imeanza kutekeleza baadhi ya ahadi ilizotoa kwa wafanyakazi wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu.

"Kati ya ahadi muhimu ambayo iliahidiwa na Rais kwa mwaka mpya wa fedha 2023/24, ni pamoja na nyongeza mshahara ya kila mwaka kwa kuzingatia miundo ya mshahara kwa kila kazi na kidato.

"Tulitarajia ahadi hiyo itatekelezwa kupitia mishahara ya mwezi Julai 2023 ambayo kwa kweli haijatekelezwa," alisema.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Mwandishi wa habari hizi alipozungumza kwa simu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alipatiwa majibu kwamba, utekelezaji wa ahadi hiyo ya serikali kwa wafanyakazi utaanza mwezi Agosti mwaka huu.

Waziri huyo alibainisha kwamba tangu kumalizika kwa Mkutano wa Bunge la Bajeti Juni 30, mwaka huu, "kuna vitu vya kitaaluma vilikuwa havijakaa sawa".

Simbachawene alisema: "Tutaanza kulipa (mishahara mipya) kuanzia mwezi ujao, kwa mwezi uliopita taratibu hazikukamilika kwa wakati kwa sababu mishahara inaanza kutolewa kuanzia tarehe 18. Tulivyomaliza Bunge, muda haukutosha.

"Kwa hiyo, tutaunganisha na malimbikizo ya mwezi waliokosa, tutajumlisha pamoja. Kwa hiyo, kuanzia mwezi ujao, wataanza kuona ongezeko la mshahara."

**AHADI YA RAIS**

Katika hotuba yake wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu, Rais Samia aliahidi kuongeza mishahara kwa wafanyakazi, akitamka:

"Kuna nyongeza za mshahara ya kila mwaka ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zimesitishwa, nikaona mwaka huu tuzirudishe.

"Kwa hiyo, wafanyakazi wote niseme kutakuwa na nyongeza ya mishahara ya kila mwaka. Tutaanza mwaka huu na tutakwenda nalo kila mwaka," alisema Rais Samia huku kukiwa na shangwe toka kwa wafanyakazi waliohudhuria sherehe hizo katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

# Hospitali yapewa bilioni 5.4/- ununuzi vifaa tiba

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imetoa Sh.bilioni 5.4 kwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na kununua vifaa tiba ili iweze kutoa huduma bora na za kisasa.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Alex Ernest, wakati akizungumza kwenye mafunzo ya menejimenti, uongozi na utawala kwa wataalamu 43 wa afya kutoka halmashauri 11 za Mkoa wa Tanga yaliyofanyika katika Taasisi ya Elimu ya Watumishi wa Afya Arusha (CEDHA).

Alisema baada ya kupokea kiasi hicho cha fedha wametumia kununua vifaa tiba pamoja kujenga miundombinu ya majengo ambayo yatatumika kutolea huduma kwa wahusika.

Hata hivyo, alisema kutokana na uwekezaji uliofanywa na serikali kwenye hospitali hiyo aliahidi kuwa kwa kushirikiana na watumishi wenzake watakuwa na usimamizi thabiti wa vifaa na miundombinu hiyo.

"Kuwa na vifaa ni kitu kimoja na kuvisimamia na kutoa huduma bora ni kitu kingine hivyo tutakwenda kusimamia ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na kwa wakati," alisema.

Mkuu wa CEDHA, Dk. Johaness Lukumay, alisema mafunzo hayo, yamefadhiliwa na Shirika la Misaada la Ujerumani la GIZ nchini Tanzania.

Dk. Lukumay, alisema taasisi hiyo ya serikali, imepewa majukumu ya kuendeleza watumishi wa afya katika kada mbalimbali.

Pia alisema taasisi hiyo inajukumu la kuwafundisha wakufunzi wa taaluma za afya ili kuhakikisha wanatoa mafunzo stahiki kwa walengwa, kufanya utafiti wa kutatua changamoto za afya na kutoa mafunzo ya muda mrefu.

Alisema: "Taasisi yetu ya CEDHA imepewa majukumu manne ikiwamo kuwaendeleza watumishi wa afya, kuwafundisha wakufunzi wa taaluma ya afya ili wakatoe mafunzo stahiki kwa walengwa, kufanya utafiti ambao utasaidia kutatua changamoto kwenye sekta ya afya na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu."


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**TAARIFA KWA UMMA**
**KUHUSU MABADILIKO YA VIWANGO VYA KODI YA MAJENGO**

**Dar es Salaam, 26 Julai, 2023:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inapenda kuutaarifu umma kuwa, Serikali imefanya mabadiliko ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289 kupitia Sheria ya Fedha ya 2023 ambapo viwango vya utozaji kodi hiyo vimebadilika pamoja na wigo wa ukusanyaji kodi hiyo umeongezeka kwa kujumuisha nyumba zilizopo maeneo yote ya Wilaya.

Viwango hivyo vya utozaji Kodi ya Majengo vilivyobadilika na ambavyo vitaendelea kutozwa kupitia ununuzi wa umeme ni kama ifuatavyo: -

Nyumba ya kawaida iliyokuwa inatozwa **shilingi 12,000/=** kwa mwaka; sasa itatozwa **shilingi 18,000/=** kwa mwaka sawa na **shilingi 1,500/=** kwa mwezi.

Nyumba za Ghorofa katika maeneo ya Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji zilizokuwa zinatozwa **shilingi 60,000/=** kwa kila sakafu kwa mwaka sasa zitatozwa **shilingi 90,000/=** kwa kila sakafu kwa mwaka sawa na **shilingi 7,500/=** kwa mwezi.

Nyumba za Ghorofa katika maeneo ya Halmashauri za Wilaya zilizokuwa zinatozwa **shilingi 60,000/=** kwa kila nyumba kwa mwaka sasa zitatozwa **shilingi 90,000/=** kwa kila nyumba kwa mwaka sawa na **shilingi 7,500/=** kwa mwezi.

Utekelezaji wa kutoza kodi hii ya majengo kwa kufuata mabadiliko tajwa hapo juu, unaanza mwezi **Julai, 2023.**

Wamiliki wa Majengo wasiotumia umeme wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wanatakiwa kufika kwenye Ofisi ya TRA iliyokaribu kwa ajili ya kupatiwa Ankara ya Malipo.

**Wamiliki wote wanaostahili kupata msamaha wa Kodi ya Majengo, wataendelea kupata msamaha huo kwa kufuata utaratibu uliokuwepo tangu awali. Baadhi ya wanaostahili kupata msamaha huo ni pamoja na wamiliki wa majengo ya ibada (Makanisa na Misikiti), majengo ya serikali, Wazee wa miaka 60 nyumba moja ya kuishi isiyotumika kibiashara, walemavu wasio na shughuli za kujipatia kipato n.k.**

Ikumbukwe kwamba, Serikali ilianza utekelezaji wa kukusanya Kodi ya Majengo kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa umeme tarehe 1 Julai, 2021 chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania ukihusisha mita za aina zote za Umeme.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea ofisi za TRA zilizopo karibu yako au wasiliana nasi kwa kupiga simu bure kwenye namba zifuatazo **0800 110 016 / 0800 750 075 (TRA) WhatsApp 0744-233 333.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***
Imetolewa na;
**IDARA YA ELIMU NA MAWASILIANO TRA**

217518302

# Tani mil. 3.7 za saruji zauzwa nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022 zinaonesha nchi kuwa na ziada ya tani milioni 3.75 ambayo imeuzwa katika soko la nje ya nchi.

Akizungumza juzi jijini hapa kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu, waziri huyo alisema saruji hiyo inauzwa katika nchi za Congo, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji.

"Hadi kufikia Juni, 2023, Tanzania ina viwanda vya saruji vipatavyo 14 ambapo kati yake, saba ni vikubwa na vilivyobakia vinazalisha saruji kutokana na 'clinker' iliyozalishwa na viwanda hivyo saba.

"Takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022, zinaonesha kuwa viwanda vya saruji nchini vinazalisha tani 10,850,000 za saruji kwa mwaka na mahitaji ya ndani ya nchi ni tani 7,100,000 kwa mwaka."

"Hivyo, kuna ziada ya tani 3,750,000 ambazo huuzwa katika soko la nje hususani katika nchi za Congo, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji," alisema.

Hata hivyo, waziri huyo alibainisha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023, uchambuzi unaonesha saruji aina ya 32.5R iliuzwa kwa ya Sh. 17,009 kwa mfuko wa kilo 50.

"Wastani wa bei ya chini ya saruji ya aina hiyo nchini kwa kipindi hicho ilikuwa ni Sh. 14,203 huku mwezi Julai 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Sh. 12,500 kwa mfuko wa kilo 50,"alisema.

Alibainisha kuwa saruji aina ya 42.5R, uchambuzi unaonesha kwa mwaka 2022/23 wastani wa bei ulikuwa ni Sh. 18,217 kwa mfuko wa kilo 50.

"Wastani wa bei ya chini katika kipindi hicho ulikuwa ni Sh. 14,917 kwa mfuko wa kilo 50 huku mwezi Julai 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Sh. 13,500 kwa mfuko wa kilo 50,"alisema.

Alibainisha kuwa wastani wa bei ya juu ni Sh. 23,800 kwa mfuko wa kilo 50 na miezi ya Aprili, Mei na Juni 2023 ikiwa na bei ya juu kuliko miezi yote kwa Sh. 24,500 kwa mfuko wa kilo 50.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama (katikati), akiwa na wanafunzi Abeli Mussa (kushoto) na Rebecca Damian (kulia), baada ya kuwapokea wanafunzi hao walioshiriki kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia kampeni ya GGML KiliChallenge 2023, inayolenga kuhamasisha uchangishaji wa fedha za mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya kina Mdee yakwama kortini

**Na Kulwa Mzee**

SHAURI la kikatiba la kupinga kuvuliwa uanachama, lililofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18, limekwama kuendelea kwa sababu mashahidi waliotakiwa kuhojiwa ambao ni wajumbe wawili wa Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA, kushindwa kufika mahakamani.

Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam iliahirisha shauri hilo jana wakati lilipokuja mbele ya Jaji Cyprian Mkeha kwa ajili ya kuwasikiliza mashahidi, Ahmed Rashid Khamis na Mary Joachim.

Wakili Hekima Mwasipu anayeiwakilisha CHADEMA, alisema wajumbe hao wameshindwa kufika mahakamani. Waliomba shauri liahirishwe hadi leo na mahakama ilikubali kufanya hivyo.

Sababu ya kutofika mahakamani inadaiwa ni mjumbe mmoja wao kuwa na changamoto kiafya na mwingine kuwa safarini.

"Shahidi Mary Joachim amepata udhuru, anaumwa, lakini shahidi mwingine Ahmed Rashid Hamis yuko njiani akitokea Zanzibar. Tumeomba ahirisho hadi kesho (leo)," alisema Wakili Mwasipu.

Wajumbe hao wanahojiwa kutokana na Maombi ya Mawakili wa walalamikaji kwa Mahakama kutaka kuwahoji na tayari Wajumbe wawili wa Bodi hiyo, Ruth Moleli na Prof. Azaveli Lwaitama walishahojiwa.

Wajumbe wengine wanaopaswa kuhojiwa ni Mary Joseph Mushi na Maulida Komu.

Kesi hiyo itaendelea leo kwa kumalizia kumhoji Ruth kabla ya kuendelea na wajumbe hao wawili.

Mdee ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) na wenzake walifungua shauri hilo kuomba mapitio ya kimahakama kupinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwafukuza uanachama wa Chama hicho.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo dhidi ya Bodi ya Wadhamini ya chama hicho, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

# Watoto walioweka rekodi kampeni ya kukabili Ukimwi wang'ara Siku ya Mashujaa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenista Mhagama amesema watoto Abel Mussa na Rebbeca Damian wenye umri wa miaka 14, walipanda Mlima Kilimanjaro kupitia kampeni ya GGML KiliChallenge-2023 na kuweka rekodi ya kipekee kutokana na mambo matatu ikiwamo kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali watoto.

Watoto hao wanaolelewa na Kituo cha Moyo wa Huruma kilichoazishwa na kufadhiliwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), walikuwa ni moja ya washiriki 61 waliopanda Mlima Kilimanjaro Julai 14 mwaka huu na kushuka Julai 20 mwaka huu.

Washiriki hao walipanda mlima huo kupitia kampeni ya GGML KiliChallenge inayolenga kukusanya fedha za kuendeleza mapambano dhidi ya VVU/ Ukimwi.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa juzi jijini Dodoma, Jenista alisema watoto hao walimwambia wamepanda mlima huo kwa kuzingatia kazi kubwa anayofanya Rais Samia katika ulinzi wa watoto wa kitanzania, haki zao na ustawi wao.

"Pia wamefanya hivyo kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na serikali katika ujenzi wa miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari na vyuo vikuu.

"Lakini pia wamesema walipanda kwa kuzingatia kazi kubwa unayofanya katika miundombinu ya afya; haya yote yakiwa na ustawi mkubwa wa watoto wote wa Tanzania," alisema.

Watoto hao ni wanafunzi wa darasa la saba; Rebecca Damiani wa Shule ya Msingi Kivukoni-Geita, alifika katika kilele cha Uhuru cha mlima huo, huku Abel Mussa wa Shule ya Msingi Mbugani, mkoani Geita, alirudia njiani baada ya kuugua malaria.

Kampeni hiyo iliyoasisiwa na GGML mwaka 2002 kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS). Mwaka huu ilishirikisha wapandamlima 35 na waendesha baiskeli 26 waliouzunguka Mlima Kilimanjaro kwa siku saba.

Akiwapokea washiriki hao, tarehe 20 Julai mwaka huu, Jenista alimwagiza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuhakikisha wanafunzi hao wanaingizwa katika orodha ya watu waliopaswa kuhudhuria Sikukuu ya Mashujaa iliyoadhimishwa juzi.

# TRA yatangaza ongezeko Kodi ya Majengo kwa Luku

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), limetangaza mabadiliko katika ulipaji wa Kodi ya Majengo kutoka Sh. 12,000 kwa mwaka kwa nyumba za kawaida iliyotozwa mwaka uliopita wa fedha hadi Sh. 18,000 sawa na Sh.1,500 kwa mwezi kwa mwaka huu wa fedha.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Elimu na Mawasiliano ya TRA kwa vyombo vya habari, ilibainisha viwango hivyo vilivyoongezeka vitaendelea kutozwa katika ununuzi wa umeme kama kawaida.

Ilifafanuliwa katika taarifa hiyo kwamba nyumba za ghorofa katika maeneo ya majiji, manispaa na halmashauri za miji zilizokuwa zinatozwa Sh. 60,000 kila nyumba kwa mwaka, sasa zitatozwa Sh. 90,000 sawa na Sh. 7,500 kwa mwezi.

Vilevile, wamiliki wa majengo wasiotumia umeme wa TANESCO, wanatakiwa kufika ofisi ya TRA iliyoko karibu nao kwa ajili ya kupatiwa ankara ya malipo.

TRA ilibainisha katika taarifa yake hiyo kuwa, wamiliki wote wanaostahili kupata msamaha wa kodi hiyo wataendelea kupata msamaha huo kwa kufuata utaratibu uliokuwapo tangu awali.

Mamlaka hiyo pia ilisema baadhi ya wanaostahili kupata msamaha huo walioainishwa ni pamoja na: wamiliki wa majengo ya ibada (kanisa na msikiti), majengo ya serikali, wazee (umri wa kuanzia miaka 60), nyumba moja ya kuishi isiyotumika kibiashara pamoja na watu wenye ulemavu wasio na shughuli ya kujipatia kipato.

Ukusanyaji wa kodi hiyo kupitia mita za TANESCO za umeme ulianza kutekelezwa nchini Julai Mosi 2021 (yaani mwaka uliopita wa fedha) chini ya usimamaizi wa TRA na TANESCO.

Ongezeko jipya la kodi hiyo limetokana na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 ambayo pamoja na mambo mengine, imeweka viwango vipya vya utozaji wa kodi hiyo kwa lengo la kupanua wigo wa ukusanyaji kodi. Inajumuisha nyumba zote zilizoko maeneo yote ya wilaya.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania ina jumla ya majengo milioni 14.34. Kati yake, ya Tanzania Bara ni milioni 13.9 na Tanzania Zanzibar ni 440,421.

**Ilifafanuliwa katika taarifa hiyo kwamba nyumba za ghorofa katika maeneo ya majiji, manispaa na halmashauri za miji zilizokuwa zinatozwa Sh. 60,000 kila nyumba kwa mwaka, sasa zitatozwa Sh. 90,000 sawa na Sh. 7,500 kwa mwezi.**

# Jela miaka 13 kwa kumkata mikono mkewe kwa panga

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mtwara imemhukumu kifungo cha miaka 13 gerezani mkazi wa kijiji cha Malopokelo mkoani hapa, Shaibu Mtepa (64), kwa kosa la kumkata mikono mke wake, Fadina Mussa.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi Fredrick Lukuna, alisema mahakama imezingatia ombi la upande wa mashtaka la kutaka kutolewa adhabu kali kwa mtuhumiwa ili kuwa fundisho kwa wengine.

Alisema hukumu hiyo pia imezingatia upande wa utetezi ulioomba mshtakiwa kupunguziwa adhabu kwa kuwa hakuisumbua mahakama, pia kuwa na umri mkubwa wa miaka 64.

Akijibu hoja ya Wakili wa Serikali Credo Rugaju ya kuiomba mahakama hiyo imuamuru mshtakiwa kumlipa fidia mlalamikaji, Hakimu Lukuna alimshauri mlalamikaji kufungua shauri la madai ili tathmini sahihi ifanyike kulingana na madhara aliyoyapata.

"Ninamshauri mlalamikaji afungue shauri la madai. Hii ni kesi ya jinai, hivyo nikisema tuingize masuala ya fidia, nina hofu nisitende haki kutokana na kutofanya tathmini sahihi ya madhara kwa mlalamikaji," hakimu huyo alifafanua.

Hakimu Lukuna alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba 3, 2021 wilayani Tandahimba kwa kumshambulia mtalaka wake kwa panga sehemu mbalimbali za mwili na kusababisha kumjeruhi kichwani, mwilini na kukatika mikono yote miwili.

Alisema siku ya tukio mlalamikaji akiwa na mashahidi, alikwenda nyumbani kwa mshtakiwa kwa lengo la kukabidhiwa baiskeli na sinki la choo ikiwa sehemu ya mgawo wa mali walizochuma wakati wa uhai wa ndoa yao.

Alisema mshitakiwa aliingia ndani na kutoka na panga na kuanza kumshambulia mlalamikaji na kumsababishia ulemavu wa kudumu.

Hata vivyo, baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mlalamikaji Fadina aliangua kilio katika viwanja vya mahakama, akidai kutoridhishwa kwa hukumu iliyotolewa. Fadina alidai hukumu hiyo haitoi fundisho kwa wanaume wenye tabia za kuwafanyia ukatili wanawake. Inachochea vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Mimi sina mikono. Nimekufa kabisa, halafu mtu anahukumiwa miaka 13. Miaka 13 kweli? Mimi sina kauli tena. Ninaomba mnisaidie kupaza sauti, Rais Samia Suluhu Hassan ninaomba uliangalie hili," alilalamika.

IITA CGIAR IRRI

**POSITION ANNOUNCEMENT**
**RESEARCHER – AGRONOMY**
**IITA-TZ-2023 - IRRI-012 -NRS- BAGAMOYO**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of **Researcher - Agronomy.**

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium.

The **Researcher Agronomy** will Facilitate the planning, designing and implementation of routine field, greenhouse and laboratory trials, data collection and analysis, and other research activities of projects on Rice production improvement and responses to abiotic stresses in Tanzania focusing on the development of improved climate resilient rice varieties, production systems. Training farmers, technicians and extension officers. Constantly communicate with internal and external project partners and collaborators to exchange conceptual ideas and to effectively gather feedback and research-related requirements for the advancement of the projects. Consolidate, evaluate and analyze research data gathered from trials, and draft reports and presentations.

**Duty Station:** The position will be based at BAGAMOYO

**Qualifications and experience**
- Master of Science in Agriculture with minimum 2 years post graduate work experience from which at least 1 year in rice research/development

**Skills and knowledge**
**mandatory**
- Has proven technical proficiency in conducting research experiments and field trials
- Has strong experience in research field, greenhouse and laboratory experiments management (layout, irrigation, fertilization, pest and disease monitoring)
- Has experience in statistical analysis and report preparation
- Has strong oral and written communication skills
- Has strong analytical skills

**Preferred**
- Has strong technical experience in guiding farmers, technicians and extension officers
- Has experience in phenotyping and assessing rice responses to different abiotic stresses and in plant physiology and/or genetics

**Responsibilities**

**1.1. Purpose**
- Undertake and supervise phenotyping of rice germplasm under different abiotic stresses, both in controlled environment facilities and in the field
- Facilitate the planning, designing and implementation of the routine trials, data analysis and other research activities of projects on rice crop improvement in Tanzania focusing on the development of improved climate resilient varieties, production systems and on training farmers, technicians, students, and extension officers.
- Contribute to the development and execution of research projects including selection of adequate research tools and equipment, verification of suggested methodologies and protocols, and accurate data collection, analyses and drafting of reports and manuscripts.
- Oversee maintenance of the research areas, research fields, technical equipment and supervise fields staff

**1.2. Engagement**
- Constantly communicate with internal and external project partners and collaborators to exchange conceptual ideas and to effectively gather feedback and research-related requirements for the advancement of research projects.
- Provide assistance and guidelines to internal and external stakeholders considering efficient implementation of the projects.
- Constantly monitor, evaluate and provide recommendations to improve research and training activities/tasks performed by Research Technicians and contract workers in order to maintain smooth conduct of field and greenhouse trials as well as to foster a productive working environment.
- Coordinate with required IRRI services and suppliers and with project partners from national research institutions and universities, to ensure smooth implantation of experiments and proper data collection, analyses and reporting.

**1.3. Delivery**
- Consolidate, evaluate, and analyze research data gathered from the project trials.
- Evaluate, validate and contribute to the interpretation of results, writing of reports, manuscripts for publications as well as presentations/posters for national and international conferences.
- Prepare and submit updated research outputs to the supervisor in a timely manner.
- Supervise and lead the maintenance of accurate data recording and updating of databases for efficient storage and retrieval of information.

**Work Condition and environment**
- Requires work in field/screenhouse/greenhouse/laboratory
- May require occasional travel within Tanzania and to other countries

**General information:**
The duration of contract for the position is three years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the **reference number for the position** as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hoja ya Samia iheshimiwe kwa ustawi wa Watanzania

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Mashujaa yaliyofanyika Mji wa Serikali wa Mtumba, Dodoma. Pia aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa mnara mpya wa Kumbukumbu ya Mashujaa katika eneo hilo.

Kwa kawaida, Siku ya Mashujaa huadhimishwa kila mwaka katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwa ni ishara ya kuwakumbuka watu mbalimbali waliojitolea katika kulitetea taifa dhidi ya uvamizi wa nchi kutoka kwa wageni. Aidha, siku hiyo huadhimishwa kuwakumbuka watu mbalimbali waliofanya mambo ya manufaa kwa taifa katika nyanja mbalimbali pamoja na kuweka alama ambazo ni kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na baadaye kwa historia ya nchi.

Katika hotuba yake kwenye maadhimisho hayo, Rais Samia alizungumza mengi lakini kikubwa zaidi alichosisitiza ni Watanzania kuendelea kudumisha umoja, amani na mshikamano miongoni mwao. Ili kufanikisha azma hiyo na kuwafanya Watanzania kuwa wamoja, Rais aliwataka wasikubali mtu au kikundi chochote cha watu kuwagawa kwa kisingizio chochote. Pia aliwataka Watanzania kuwaenzi mashujaa waliojitoa kwa damu na jasho katika kutetea taifa kwa kudumisha amani, umoja na mshikamano miongoni mwao ambavyo ni tunu ya taifa. Mbali na kudumisha tunu hizo, aliwasihi Watanzania kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo binafsi, ya familia na taifa kwa ujumla.

Wito huo wa kiongozi mkuu wa nchi umetolewa huku Watanzania wakishuhudia kauli kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo wanasiasa na wanasheria kuhusu sakata la bandari huku baadhi ya wahusika wakiugusa Muungano ulioasisiwa na viongozi wa kwanza wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume. Suala hilo, katika mjadala wa wahusika hao, inagusa masuala ya Tanganyika na Zanzibar jambo ambalo linaibua nyufa na hata kuashiria kutikisika kwa taifa.

Kama alivyosema Rais, makundi yanayovutana kuhusu hoja hiyo wasitumike kuwagawa Watanzania kwa misingi ya maeneo yao, itikadi zao wala imani zao. Sambamba na hilo, sakata la bandari lisiwe kisingizio cha kuwagawa Watanzania.

Pia ni vyema ikafahamika kwamba suala la bandari kama ambavyo limeshika hatamu katika mijadala sasa, si la kwanza kutokea ndani ya Tanzania. Yako mambo mengi ambayo yalijitokeza yakiwamo Zanzibar kujiunga na Jumuiya ya Kiislamu Duniani (OAC) ambalo lilisababisha Bunge kuwaka moto. Hata hivyo jambo hilo lilimalizika kwa amani licha ya kwamba lilitishia kuvunjika kwa Muungano baada ya kundi la wabunge, maarufu kama G55 kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika. Yanapotokea mambo kama hayo, kumekuwa na utamaduni wa kuyamaliza ama kuyatatua kupitia vikao au majukumu mbalimbali vilivyowekwa kikatiba. Miongoni mwa majukumu hayo ni vikao ndani ya vyama au kamati mbalimbali na matokeo yake hali ya amani na utulivu hurejea na watu kuendelea kuishi kwa usalama na kama ndugu.

Kwa muktadha wa sasa, suala la bandari nalo linaweza kumalizwa kwa hekima na busara badala ya kuendelea kuibua malumbano na baadhi ya watu kutoa lugha za matusi na za kuudhi. Pia suala hili linapojadiliwa, watu wajielekeze katika hoja na si kushambuliana kwa misingi ya u-Tanganyika na u-Zanzibari kama ilivyo sasa jambo ambalo linaweza kuleta sintofahamu kwa misingi ya pande za Muungano.

Ni vyema pande zinazohusika na mjadala wa suala hili zikatambua kwamba amani, utulivu, umoja na mshikamano vilivyoko nchini kwa sasa vinatokana na misingi ya watu kuishi kwa kuheshimiana na kutumia lugha za staha, hivyo jambo hilo lisiondoe misingi hiyo kwa ustawi wa taifa.

Kama alivyosema Rais Samia kuwa Watanzania wasigawanyike kutokana na kisingizio chochote au kikundi cha watu, hakika kila mtu aheshimu kauli hiyo na kama kuna hoja yoyote ya msingi inaibuliwa, ijibiwe kwa hoja na si kutumia nguvu, vitisho na kurushiana lugha za matusi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kundi hili ni muhimu tulilinde zaidi

**VIJANA** wa rika balehe kuanzia miaka 14 hadi 24, wamekuwa wakijihusisha na matendo yanayoweza kuwaingiza katika hatari ya kuambikizwa magonjwa, huku wengine wakipata mimba za utotoni na kushindwa kutimiza ndoto zao kielimu na kiuchumi.

Lakini afya ya uzazi kwa vijana hao, inatajwa kuwa muhimu, kutokana na ukweli kuwa inaweza kuwafanya wawe salama na kuepuka vikwazo wanavyokumbana navyo ambavyo wakati mwingine vinaweza kuwasababishia vifo.

Kwa hali hiyo, elimu ya afya ya uzazi kwa vijana waliopo shuleni na wasio madarasani ni muhimu kutokana na ukweli kwamba wengi wanajihusisha na vitendo vya ngono katika umri mdogo.

Elimu hiyo ni ile ya malezi na makuzi kwa makundi rika, pamoja na kutunga sheria ndogo za kuzuia ngoma zenye mmomonyoko wa maadili na ushawishi wa zinaa kama vigodoro ili kumlinda mtoto na kumwezesha kusoma.

Kimsingi, taifa linahitaji nguvu kazi ambayo ni vijana, hivyo ni muhimu wakapata elimu rika na ujinsia ili waweze kujitambua na hatimaye wafikie malengo yao kwa manufaa ya jamii inayowazunguka na Taifa kwa ujumla.

Hivyo, afya kwa vijana balehe ni msingi mzuri wa kuyafikia malengo mengine yakiwamo ya maendeleo endelevu. Na njia nzuri ya kuboresha ndoto zao za kuwapa elimu ya malezi na makuzi kwa makundi rika.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu hiyo, serikali ya Tanzania na Tanzania, zimeingia makubaliano ya ushirikiano ya kuboresha afya za vijana balehe nchini kupitia mradi wa shirika uitwao 'Nutrition International'.

Ni Julai 20 mwaka huu jijini Dodoma Waziri wa Afya Ummy Mwalimu na Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Canada, Harjit Sajjan, wanatangaza kuanza kwa mradi huo, katika hatua hiyo, kazi itafanyika kwa miaka saba, itatekelezwa mkoani Tabora na shirika la Nutrition International kwa kushirikiana na Engender Health na Young and Alive Initiative.

Aidha, serikali ya Canada imetoa Dola za Marekani milioni 15 kwa ajili ya kuboresha afya ya wasichana ambao ni wazi wanakabiliwa na vikwazo vingi katika maisha yao, kwa mfano, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwahi kukariri takwimu za Elimu Msingi Tanzania (BEST - 2020), kuwa hadi kufikia Desemba mwaka 2020, wanafunzi 6,475 walipata mimba na kuacha shule.

Anafafanua kuwa katika idadi hiyo, wanafunzi wa shule za msingi ni 1,135 na 5,340 wa sekondari, lakini pia kundi hilo la vijana balehe linakabiliwa na magonjwa ya kuambukizwa, upungufu wa taaluma za ajira, matumizi ya dawa za kulevya, ukatili wa kijinsia, ndoa za utotoni.

Kwa hali hiyo, ni wazi jamii kuhusika na ulinzi wa watoto kwa kuweka mipango itakayoondoa mazingira yanayowafanya vijana balehe kuwa na tamaa ya vitu na kushawishika kujiingiza katika ngono wakiwa na umri mdogo ni muhimu.

Sio siri kwamba mimba za utotoni na mambo mengine yanayosababishwa na rika balehe vimekuwa mwiba kwa kipindi kirefu na zinawanyima vijana wa kike na wa kiume na kuwanyima fursa za kutimiza malengo yao.

Hivyo, ninaamini kuwa kwa utaratibu ambao Wizara ya Afya imekuja nao kwa kushirikisha wadau kutoka Canada, unaweza kuwasaidia vijana kulinda afya zao na kufikia malengo waliojiwekea katika maisha.

Ikumbukwe kuwa maisha yenye afya kwa vijana ni muhimu, kwani bila afya, itakuwa vigumu kuyafikia malengo mengine ya maendeleo endelevu yanayoelekezwa na Umoja wa Mataifa.

HABARI KITAIFA

# Ndege ya mizigo ATCL yasafirisha tani 26 za chanjo kuelekea DRC

**Na Joseph Mwendapole**

NDEGE ya mizigo ya Boieng 767-300F ya Shirika la Ndege Tanzania ya (ATCL), imesafirisha tani 26 za shehena ya chanjo kuelekea Congo DRC ikiwa ni safari yake ya tano tangu inunuliwe kutokea nchini Marekani.

Shehena hiyo ni mali ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia watoto (UNICEF). Iliondoka kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), majira ya saa tano asubuhi na kutarajiwa kuwasili nchini Congo DRC saa nane mchana.

Akizungumza kwenye uwanja huo jana, Meneja Huduma za Viwanja vya Ndege wa (ATCL), Edward Mkwabi alisema, uwezo wa ndege hiyo ni kubeba tani 54 za shehena na ina uwezo wa kukaa angani kwa saa 10 bila kutua.

"Leo tumepata fursa ya kusafirisha mizigo kwa kutumia ndege yetu, huu mzigo umetoka India ni chanjo imekuja hapa Tanzania kuunganisha kwenda DRC hii ni safari yetu ya tano tunasafirisha mizigo tangu ndege yetu iwasili nchini," alisema.

Alisema tangu iwasili nchini ndege hiyo imefanya safari za kupeleka mizigo kwenye mataifa mbalimbali ikiwamo Dubai.

"Ndege hii ina uwezo wa kudhibiti hali ya joto au baridi, sasa kwa bidhaa kama hii tunayosafirisha leo ni muhimu kuwa na ndege kama hii ili kuhakikisha bidhaa ya mteja inasafirishwa bila kupata changamoto ya aina yoyote," alisema.

Alisema kwa muda mrefu wanasafirisha mizigo kwa kutumia ndege ya shirika hilo aina ya 787 Dreamliner ambayo ina uwezo mkubwa wa kubeba mizigo na abiria.

"Tuna uwezo mkubwa wa kubeba bidhaa kama hizi ndiyo sababu tunawaambia Watanzania wenye shehena mbalimbali wasiache kutumia ndege ya shirika lao kusafirisha mizigo kwenda kwenye maeneo mbalimbali duniani," alisema.

Alisema, ingawa kuna ushindani mkubwa kwenye biashara ya kusafirisha mizigo, lakini ndege hiyo ya Boeing 767-300 imekuwa kivutio kwa wafanyabiashara wengi kutokana na kusafirisha mzigo mkubwa wa aina yoyote bila kuharibika.

Alisema nia ya serikali kununua ndege hiyo ni kuchochea usafirishaji wa bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini kwenda nje ya nchi na kuwarahishia wanaoagiza bidhaa nje ya nchi kuzileta nchini kwa gharama nafuu.

Alisema ATCL pia inatoa huduma ya kusafirisha mizigo ya kuunganisha inayotoka mataifa mbalimbali kuja Tanzania kwa kupeleka mizigo hiyo kwenye nchi jirani ambazo hazina ndege ya mizigo kama ya shirika hilo.

John Lupemba, ambaye ni mdau wa kusafirisha mizigo kwa njia ya anga, aliipongeza ATCL kwa hatua kubwa ya kusafirisha mizigo ambayo kwa miaka ya nyuma ilichukua muda mrefu kuwafikia walengwa wa maeneo mbalimbali.

Alisema, awali huduma ya usafirishaji mizigo kwa njia ya anga haikuwa rafiki kutokana na gharama kuwa kubwa kwa uhaba wa ndege za mizigo.

"Gharama zilikuwa juu sana kwa mfano ukitaka kusafirisha mzigo unakodi ndege, sasa gharama zilikuwa zinamwangukia mteja lakini kwa sasa tunashukuru kwamba tuna ndege ambayo tunasafirisha bidhaa kwa gharama nafuu," alisema.

# Mstaafu JWTZ ataka Mkoa Tabora kupewa hadhi

**Na Benny Kingson,** TABORA

ASKARI mstaafu wa Jeshi la Wananchi nchini (JWTZ) Sajenti Amon Saliboko, ameishauri serikali kwa kuwaenzi mashujaa waliopambana kupigania uhuru wa taifa na vita ya kumng'oa Nduli Iddi Amini na Mkoa wa Tabora kuupa hadhi na heshima inayostahili kutokana na chimbuko la harakati za ukombozi wa uhuru wa Watanzania kufanyikia mkoani humo.

Sajenti Saliboko aliiambia Nipashe kuwa ipo haja kwa serikali kuufanyia marekebisho makubwa mnara wa mashujaa Tabora pamoja na eneo ilipo sanamu ya Mwalimu Nyerere ili upate mwonekano na hadhi inayostahili.

"Hapa ndipo pana historia ya mashujaa waliopigania uhuru wa nchi na sio mnara wa kumbukumbu ya vita kama inavyosemekana na kwamba kuna makaburi, mnara huu umewekwa hapa kwa kuwa Baba wa Taifa hayati Mwalimu Nyerere ndipo alipohutubia na kutoa machozi akidai uhuru wetu na zikapigwa kura tatu za maamuzi ya busara," alisititiza.

Askari huyo mstaafu aliyepigana vita ya kumng'oa Nduli Iddy Amini Dada, alisema Mkoa wa Tabora una historia ya pekee katika nchi hivyo serikali inapaswa kuutazama kwa jicho la karibu na kuutendea haki kwa kuufanya uwe na hadhi na heshima kubwa kuliko ulivyo hivi sasa.

"Natambua zipo jitihada zimefanywa na wazee wa Tabora za kuitaka serikali kufanya maboresho eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuweka maktaba ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, kulifanya kuwa kivutio eneo la mapumziko na kitega uchumi kurudi kama ilivyokuwa awali ambapo kwa sasa vimekufa na kutelekezwa," alisema.

Pia, alisema kuna kila sababu ya serikali kusikiliza hoja za wazee walizozitoa kuhusu kutaka mkoa huo kukumbukwa, kuenziwa na kupewa hadhi inayostahili na kufanyiwa maboresho maeneo yote nyeti yenye historia kwa faida ya vizazi vilivyopo na vijavyo pamoja na kuwavutia watalii.

Hivi karibuni wazee wa Tabora walifanya mkutano wa hadhara na wakamuita Mkuu wa mkoa aliyewakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Louis Bura, kumpa maoni yao kuhusu maboresho ya eneo la sanamu ya Mwalimu Nyerere, mnara wa kumbukumbu ya mashujaa hao unaodaiwa kumilikiwa na JWTZ badala ya manispaa hiyo.

Wazee hao pia walitaka Sh. milioni 90 zilizotengwa kukarabati eneo la PPP zipelekwe kukarabati eneo la sanamu hiyo lililotengewa Sh. milioni 30 ambazo pia zinadaiwa kugemwa Sh. milioni 10 kupelekwa kujengea mabanda ya wamachinga.

Aidha, walitaka uwanja wa mpira Vita uanaodaiwa kumilikiwa na JWTZ ambao umeandikwa maandishi kwenye kuta za uwanja huo ukionyesha ni wao, urejeshwe kwa manispaa.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
## TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

## TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'

**1. UTANGULIZI:**

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa Wanawake na Vijana, na Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo Yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** 28/08/2023 – 22/09/2023 | **ICoT – Mbeya** |
| 2 | Kozi ya Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (10)** 09/10/2023 – 16/12/2023 | **ICoT – Mbeya** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

A. **Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana:** Washiriki watajifunza mada mbalimbali kuhusu ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya Barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kuwawezesha Wanawake na Vijana (Washiriki) kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

B. **Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads):** Washiriki watajifunza mada mbali mbali kuhusu mbinu za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, watajifunza mada mtambuka ambazo zitahusu utaratibu wa namna ya kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara pamoja na Usimamizi wa kazi za Barabara.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**

Mafunzo yote yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa ni ya nadharia Darasani na awamu ya pili itakuwa ni ya mafunzo kwa vitendo.

**4. MALENGO YA KOZI**

Kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'. Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbalimbali za ujuzi na weredi wa kufanya Matengenezo, Ukarabati na usimamizi wa kazi za Barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika maeneo yafuatayo: -

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za Changarawe/Udongo; na
iii. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani **"SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS"** kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO: -**

Walengwa wa mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ni kama wafuatao: -

i. Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
ii. Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
iii. Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
iv. Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
v. Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO: -**

Lugha itakayo tumika katika kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki kumi (10) ni Kiingereza; kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

a) **Kozi ya ukarabati na matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe (Wiki 10)**
i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 800,000; na
ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,600,000.

b) **Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana (Wiki 4)**
i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 400,000; na
ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 700,000

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI: -**

Washiriki watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi mbili zilizotajwa hapo juu wanaombwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA TAASISI**

| | |
|---|---|
| **Institute of Construction Technology**<br>**ICoT,**<br>**S.L.P 963, MOROGORO.**<br>**Simu : 023- 2935229/023- 2935226**<br>**: 0762 409087/0786 384 062**<br>**Nukushi : 023-2935227**<br>**Barua pepe : mwti@morogoro.net** | **Institute of Construction Technology**<br>**ICoT,**<br>**S.L.P 1957, MBEYA.**<br>**Simu : 025 295 7484/5**<br>**: 0787 059 555/0769 317 404/ 0765 251 509**<br>**Nukushi : 025 295 7486**<br>**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz,**<br>**attimbeyafrica@gmail.com** |

# Jamii yatakiwa kuandika wosia kuepusha migogoro

**Na Ibrahim Joseph,** RUVUMA

JAMII imetakiwa kuandika wosia kwa Warithi wa Mali zao mapema wakiwa hai ili kupunguza migogoro ya Familia kugombea Mali za Marehemu.

Wakili wa Serikali Wizara ya Katiba na Sheria, Irene Nyantory, alisema hayo wakati wa mwendelezo wa utoaji Elimu kupitia Kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia iliyofanyika, Manispaa ya Songea, Mkoani hapa jana.

Nyantory aliiasa jamii kuondoa Imani potofu kuwa kuandika wosia mapema ni kujichulia kifo bali watu wanachotakiwa ni kuandika wosia huo mapema wakati wa uhai ili kuondoa migogoro.

Alibainisha kuwa wosia mara nyingi unaonesha nani atakuwa Mrithi wa Mali za Marehemu na atazikwa wapi kuondoa migogoro hiyo ambayo huzigawa Familia kwa kugombea Mali.

Alisema migogoro imekuwa mingi na kusababisha mifarakano katika Familia na wakati mwingine husababisha madhara kwa wahusika hasa Watoto na Wanawake.

Kadhalika, alisema wosia huo unaweza ukawa wazi au siri na ukiandikwa unaweza kuhifadhiwa kwa Wakili, Wakala wa usajili, ufilisi na udhamini (RITA) kwa Waumini wa Dini ya Kikrsto wanaweza kuhifadhi Kanisani na Waumini wa Dini ya Kiislamu wanaweza kuhifadhi msikitini.

Alisema utaratibu wa kuandika wosia kwa siri unasaidia kupunguza malalamiko kwa mhusika kudaiwa kuwa amependelea baadhi ya watoto au wanafamilia.

Pia, alisema wosia unaweza ukawa wa wazi kulingana na mhusika anavyoona kuwa hali ikoje kwenye Familia yake iliyopo na wakijua hufanya waishi kwa amani bila migogoro.

Alisema kupitia kampeni hiyo wanatoa Elimu kwa Wananchi kuhusu jinsi ya kupata Haki zao pamoja na kujua namna ya kutafuta haki zao kwenye Vyombo vya maamuzi na Kisheria.

Nyantory alisema pia kampeni hiyo inatoa nafasi kwa Wananchi wa maeneo husika kukutanishwa na Wataalamu wa Kisheria, Ardhi na Maendeleo ya kijamii mbalimbali waliopo kwenye timu hiyo na kusaidiwa tatizo lake.

Askari kutoka dawati la kijinsia Jeshi la Polisi kituo cha Songea, Sajenti Mwanaisha Ndauka, alisema matukio mengi yanayoripotiwa kwao ni kinamama kunyanyaswa na waume zao vipigo na kunyanyaswa kiuchumi kwa wanaume kuuza mali za kilimo bila kugawana na familia.

Sajenti Ndauka alisema wanapokea matukio ya Ubakaji na Ulawiti, lakini jeshi hilo limekuwa likisaidia kwa wahusika kwa vitendo hivyo kukamatwa ili mkondo wa sheria kufanya kazi yake.

Mkazi wa mtaa wa Makambi, Omari Habibu alisema kuna umuhimu wa wazazi kuandikishana kwa Mwanasheria na Warithi wao ili kuepuka kugeukana baada ya muda.

"Mimi binafsi baba yetu alitugawia mashamba huko kijijini kwetu Namtumbo tukapanda miti, lakini baada ya muda alitugeuka na kuanza kuuza mashamba hayo bila kutushirikisha na umri wake sasa ni miaka zaidi ya 90," alisema.

Habibu alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuandika wosia na kuandikishana kwa Mwanasheria au viongozi wa maeneo husika ili kuondoa migogoro kwenye familia.



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu akizungumza na viongozi wa chama hicho wa kata zote 20 za jimbo la Lindi mjini juzi, wakati akiwa katika ziara yake ya kuimarisha chama mkoani Lindi hivi karibuni.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanasiasa waonywa kufedhehesha viongozi wa dini

**Na Moshi Lusonzo**

WANASIASA wa vyama mbalimbali nchini wameaswa kuacha kutumia lugha ya maudhi na inayowafedhehesha viongozi wa dini wakati wanapoikosoa serikali.

Akizungumza jijini Dar es Sakaam jana, Shekhe wa Wilaya ya Temeke na Mwenyekiti wa Kamati ya Amani wa wilaya hiyo, Zailai Hassan, alisema vitendo vinavyoibuka sasa vya wanasiasa kutoa lugha isiyofaa kwa viongozi wa dini katika mikutano yao ya kisiasa havikubaliki na vinatakiwa kulaaniwa.

Alisema wanasiasa hawapaswi kuwaingiza viongozi wa dini katika jambo lolote la kisiasa kwenye mikutano yao, ili kuepusha kuvunjika kwa amani nchini.

"Tunawaomba wanasiasa wote kuacha kutumia lugha ya kuwadhalilisha viongozi wa dini, jambo hili likiendelea linaweza kuleta hatari na hatupaswi kunyamaza viongozi wetu wa dini wakidhalilishwa kwenye majukwaa," alisema.

Aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, alinukuliwa akikemea viongozi wa dini kwa kuogopa kuhudhuria mkutano wa chama cha Chadema, kwa madai ya kutishwa kuzungumzia sakata la Bandari.

"Hakuna anayekatazwa kukosoa jambo lolote la serikali, lakini wanapoingizwa viongozi wa dini na kudhalilishwa mbele ya waumini wao siyo jambo la kufurahia, lazima tulilaani kwa nguvu zote na mwanasiasa yeyote aache mara moja," alisisitiza Shekhe Hassan.

Mwenyekiti wa vijana wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Dar es Salaam, Sharifu Kasobwe, alisema Katiba ya nchi na taratibu za Watanzania viongozi wa dini wanaheshimika na ndiyo wanatumika katika shughuli mbalimbali za kitaifa na hivyo kuwaingiza katika siasa ni kosa.

"Kukosoa jambo siyo dhambi, lakini kinachokosewa ni njia inayotumika. Lazima umakini unatakiwa kwa sababu unapokwenda kinyume na kuwashambulia viongozi wa dini zetu kwa sababu tu hawakufikia malengo yako tunakosea," alisema Kasobwe.

Aidha, Khalifa Athumani, alisema kinachoendelea sasa kila mtu anayetaka kujadili ahakikishe anatumia maneno ya staha kwa ajili ya kuepuka madhara yatakayotokea ndani ya jamii.

## PURA kujenga madarasa mapya Shule Likong'o Lindi

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Charles Sangweni, amesema Mamlaka hiyo inafuatilia kwa karibu Mwongozo wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), kwa kampuni za mafuta ikiwamo ujenzi wa madarasa mapya katika Shule ya Msingi Likong`o mkoani Lindi.

Sangweni alisema hayo wakati akielekea kwenye ziara ya kikazi mkoani Mtwara na kutembelea shule hiyo kujionea hatua zilizofikiwa katika mpango wa ujenzi wa madarasa mapya kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), na wabia wake.

Sangweni alisema mwongozo wa CSR ni miongoni mwa mambo yaliyopangwa kufanyiwa kazi mwaka huu kama ilivyoainishwa katika mipango yao ya uwajibikaji na alifanya mazungumzo na Diwani wa Kata ya Likong'o, wajumbe wa kamati mbalimbali za serikali za mtaa katika Kata, pamoja na baadhi ya viongozi wa shule hiyo.

"Ujenzi wa madarasa mapya katika shule hii ni jambo ambalo limechukua muda mrefu tangu kuanza kufanyiwa kazi. Ni matamanio yetu kuona utekelezaji unafanyika mwaka huu na ndiyo maana tumeamua kulifuatilia kwa karibu," alisema Sangweni.

"Eneo la Likong'o lililopo Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ndipo ambapo mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG) utatekelezwa. Mradi huo unakadiriwa kuwa na uwekezaji wa takriban Sh. trilioni 97 ukitarajiwa kuleta fursa nyingi kwa Watanzania kama vile ajira na utoaji wa huduma mbalimbali wakati wa ujenzi na uendeshaji wa mradi, kwa hiyo tunatamani na miradi hii midogo ya shule ikamilike ili wananchi nao waone fahari ya mradi."

Diwani wa Kata ya Mbanja, Thabiti Ngwame, alisema kuwa suala la ujenzi wa madarasa katika shule hiyo linapaswa kufanyiwa kazi na kufika tamati kwa kuwa ni suala ambalo limekuwa na mlolongo usioisha.

"Tunatamani utekelezaji katika ujenzi wa shule hii ufike mwisho sasa maana limechukua muda mrefu, mlolongo wa kukamilisha taratibu za kuanza utekelezaji umekuwa mrefu sana," alisema Ngwame.

Mkuu wa shule hiyo ya Likong`o, Shafii Said, alipendekeza ujenzi wa madarasa hayo uanze mapema kwa kuwa yale yaliyopo kwa sasa hayapo katika hali nzuri.



# Mil.584/- kukamilisha ujenzi Shule ya Sekondari Moivo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetoa Sh. milioni 584.2 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Moivo, iliyoko katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru ili kurahisisha upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wa eneo hilo.

Fedha za ujenzi wa shule hiyo zimetolewa na serikali kupitia mradi wa kuboresha miundombinu ya elimu kwa shule za sekondari (SEQUIP), lengo likiwa ni kuweka mazingira rafiki ya kufundishia kwa walimu na kujifunzia kwa wanafunzi.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Pamoja na mambo mengine alikiri kupokea kiasi hicho cha fedha kwenye akaunti mama ya Shule ya Sekondari Enyoito na tayari kwa ajili ya mchakato wa ujenzi kuanza.

Alisema kuwa kiasi hicho cha fedha kitatumika kujenga vyumba vinane vya madarasa, maabara tatu za masomo ya sayansi, chumba cha somo TEHAMA, ujenzi wa matundu nane ya vyoo yenye sehemu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na chumba maalum cha wasichana kubadilishia nguo wakiwa kipindi cha hedhi.

“Kama ilivyokuwa utaratibu wa serikali ujenzi huu, utatekelezwa kwa kuwatumia mafundi jamii na shughuli zote zitafanyika kwenye ngazi ya jamii kwa usimamizi wa wataalamu wa ofisi yangu,” alisema.

Hata hivyo, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu kwa kutoa fedha hizo kwa kuwa zimepelekwa wakati muafaka kwa Kata ya Moivo.

Alisema kata hiyo ina idadi ya kubwa ya wanafunzi ambao wanakwenda kutafuta elimu katika kata za jirani za Ilkiding’a na Enyoito jambo ambalo limesababisha msongamano wa wanafunzi darasani kwenye shule hizo.

Naye Ofisa Elimu Sekondari, Halmashauri ya Arusha, Menard Lupenza, alisema kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo kutawasaidia wanafunzi wa eneo hilo kwenda shuleni karibu na makazi yao.

Pia alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutasaidia kuondoa msongamano wa wanafunzi kwa shule za jirani pamoja na kurahisisha tendo la kujifunza na kufundisha kwa wanafunzi na walimu na kupandisha kiwango cha taaluma shuleni hapo.

Alisema: “Kutokana na serikali kutoa elimu bila malipo kumekuwapo na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari, hivyo kuna uhitaji wa shule za sekondari kwenye kila kata”.

# Wakili akoleza vita dhidi ya ukatili wanawake, watoto

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKILI Elizabeth Minde, amekoleza vita dhidi ya ukatili wa wanawake, watoto wanaoendelea kuathiriwa na vitendo hivyo ambavyo vinahatarisha uhai wa taifa, akilitaja Jeshi la Polisi, Maendeleo ya Jamii na watendaji wa kata kutokubali nguvu kazi ya taifa kunajisiwa na vitendo hivyo.

Hivyo amewapa mbinu za kimkakati za namna wanavyoweza kuvidhibiti na kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na wale walioathiriwa na vikwazo vya unyanyasaji wa kitamaduni na mijadala katika jamii za vijijini na mijini.

Minde aliwapa mbinu hizo jana alipokutana na makundi hayo yaliyoshiriki kutengeneza mpango kazi wa utekelezaji wa mradi mpya uliobatizwa jina ‘jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Mradi huo wa miezi sita, unatekelezwa katika kata tano za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro na Shirika la KWIECO kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust).

“Polisi wana nafasi yao lakini sisi tunajaribu kusema matukio haya yapo, hayaibuliwi. Mengine yanafunikwa kule nyumbani, ni kwa sababu tu ya mifumo na mitazamo tuliyonayo.

.Amebakwa mtu, unaambiwa si mkazungumze muelewane? ndiyo kesi nyingi huwa zinakufa kwa mtindo huo na hazifiki mbele zinafia njiani.

“Kwa hiyo tukubaliane kwamba kazi tunayoifanya ni kazi ambayo tunapambana na mfumo ambao hauwezi kuubadilisha kwa siku moja, haiwezekani. Nawasihi wapambanaji wote kwenye vita hii tusikubali matukio haya yaendelee kunajisi nguvu kazi ya taifa. Mmesikia kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka huu, wanawake ndio wengi.”

Akizungumza wakati wa kuutambulisha mradi huo kwa wadau wanaoshiriki vita hiyo, Mratibu wa mradi huo, Veronica Ullomi, alisema kata ambazo zimelengwa ni Mwika Kaskazini, Mwika Kusini, Oldmoshi Magharibi, Kibosho Magharibi na Kirua Vunjo Kusini.

Alisema mradi huo unalenga kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya kiakili yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Kilimanjaro.

Aidha, mradi huo unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Vilevile, unalenga kuhimiza haki na haki za elimu kwa watoto wa kike kwa kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi yao vinatokomezwa na jamii iwe mstari wa mbele kuhimiza na kusaidia wasichana kuingia tena katika mifumo rasmi ya shule.

## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2023.

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2023 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2023 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 713.63 | 1,068.65 |
| 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 5,387.60 | 4,758.64 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 36,721.28 | 38,309.57 |
| 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,373.88 | 1,243.50 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 100.10 | 65.27 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 7,641.61 | 7,780.46 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 50,836.69 | 53,427.82 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,677.66 | 1,596.44 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 959.44 | 1,053.94 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **105,411.89** | **109,304.29** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 8,207.50 | 11,625.00 |
| 18 | Amana za Wateja | 53,867.90 | 54,239.59 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,609.81 | 1,591.77 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 669.79 | 927.65 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **64,355.00** | **68,384.01** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **41,056.90** | **40,920.27** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 557.45 | 595.37 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,254.41 | 7,216.49 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 415.04 | 278.42 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,056.90** | **40,920.27** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 6,886.70 | 7,522.08 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 669.25 | 1,267.77 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 204.41 | 91.14 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38.95% | 37.44% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.31% | 2.37% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82.20% | 81.23% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 48.23% | 48.88% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.62% | 92.18% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -5.75% | 4.02% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -3.56% | 2.60% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2023 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Juni 2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2023 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,120.77 | 2,089.88 | 4,234.02 | 4,588.71 |
| 2 | Gharama za Riba | 791.75 | 824.05 | 1,595.61 | 1,684.45 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,329.02** | **1,265.83** | **2,638.41** | **2,904.26** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 113.27 | (18.50) | 123.75 | (11.25) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **94.51** | **202.51** | **301.78** | **323.44** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 34.70 | 55.52 | 82.93 | 117.44 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 59.80 | 146.99 | 218.86 | 206.00 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,018.64** | **1,088.63** | **1,961.41** | **1,932.97** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 374.59 | 483.95 | 797.35 | 850.41 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 5.71 | 5.94 | 11.57 | 11.77 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 638.33 | 598.74 | 1,152.48 | 1,070.80 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **291.62** | **398.22** | **855.04** | **1,305.98** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 155.00 | 233.33 | 440.00 | 533.33 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **136.62** | **164.89** | **415.04** | **772.64** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 25 | 24 | 25 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 4 | 5 | 13 | 24 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 4 | 5 | 13 | 24 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.51% | 0.54% | 0.77% | 1.23% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.33% | 1.61% | 2.03% | 3.78% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 71.56% | 74.14% | 66.71% | 59.89% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.40% | 4.49% | 5.30% | 5.02% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2023.

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2023 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2023 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2022 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 136.62 | 278.42 | 136.62 | 772.64 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 96.03 | 95.97 | 96.03 | (216.90) |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 2,591.13 | (3,382.64) | 2,591.13 | 3,773.53 |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | (3,789.20) | 2,545.86 | (3,789.20) | (13,115.94) |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (11.26) | 313.15 | (11.26) | 810.88 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (526.65) | 215.01 | (526.65) | (2,254.81) |
| Kodi iliyolipwa | (155.00) | (285.00) | (155.00) | (533.33) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(1,658.32)** | **(219.23)** | **(1,658.32)** | **(10,763.92)** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (1.54) | (0.55) | (1.54) | 329.07 |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (1,988.09) | 5,553.31 | (1,988.09) | (10,422.54) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(1,989.63)** | **5,552.75** | **(1,989.63)** | **(10,093.47)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (66.32) | (82.27) | (66.32) | (136.80) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(66.32)** | **(82.27)** | **(66.32)** | **(136.80)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (3,714.26) | 5,251.26 | (3,714.26) | (20,994.19) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 17,337.24 | 12,085.98 | 17,337.24 | 47,101.31 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **13,622.97** | **17,337.24** | **13,622.97** | **26,107.11** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/06/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 415.04 | - | - | - | **415.04** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (89.75) | 89.75 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **7,669.45** | **557.45** | **-** | **-** | **41,056.90** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 895.43 | - | - | - | **895.43** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 811.68 | (811.68) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2023


Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 26-07-2023 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 26-07-2023 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 26-07-2023 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 26-07-2023 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 26-07-2023 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**





# Wachimbaji waiangukia serikali kufukuzwa maeneo yao

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika mgodi wa tambalale namba mbili Mwazimba uliopo katika Kata ya Chele mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuwasaidia kupata haki zao baada ya kutakiwa kuondoka kwenye machimbo hayo.

Wachimbaji hao walitakiwa kuondoka kwenye eneo hilo baada ya kampuni ya uchimbaji madini ya Amani Gold Mining kupatiwa leseni ya uchimbaji katika eneo hilo bila maelewano na wachimbaji hao walioanzisha machimbo hayo.

Akizungumzia Nipashe juu ya sakata hilo mmoja wa wachimbaji hao ambaye ni mmiliki wa maduara ya uchimbaji, Silas Maige alisema wamekuwa wakijishughulisha na uchimbaji wa mdaini katika eneo hilo tangu mwaka 2018 na leseni imetolewa mwaka 2020.

Alisema wakati huo wao walikuwa tayari wana hati ya kikundi cha Nyawisolele Gold Mine na kuwa wao ndiyo waliogundua uwepo wa madini ya dhahabu katika eneo hilo lakini serikali imetoa leseni na kuwataka kuondoka.

Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo, Christopher Mtiriga alisema katika eneo hilo wachimbaji wamewekeza kwa kuchimba maduara 58.

Alisema eneo hilo lina wawachimbaji ambao wamewekeza nguvu na wengine wanauza nyumba na mali zingine na kuwekeza fedha hizo katika kuchimba maduara hayo lakini wamepewa notisi ya kuanzia Julai 6 hadi Agosti 27. "Eneo hili lina zaidi ya wachimbaji wadogo 120 ambao wote familia zao zinategemea katika shughuli hiyo tu na bado walikuwa wakichimba na kulipa mrahaba serikalini pamoja na kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo," alisema. Mwenyekiti wa wamiliki wa maduara, Gerlad Bahebe aliiambia Nipashe kuwa wakurugenzi na wamiliki wa leseni ya Amani Gold Mine wameingia ubia na mwekezaji na kutoa fidia au kifuta jasho cha Sh.milioni sita kwa mduara mmoja, kwamba miduara mingine hayatambui.

Nipashe ilimtafuta mmoja wa wakurugenzi wa Amana Gold Mining, Leonard Barnaba ambaye alisema kuwa tayari ameanza kufanya makubaliano na baadhi ya wamiliki wa maduara na watalipa Sh.milioni sita kwa kila duara na tayari wamelipa zaidi ya Sh.milioni 60.

Nipashe ilimtafuta Ofisa Madini Mkazi wa Wilaya ya Kahama, Jeremiah Hango ambaye alisema kuwa wamiliki wa leseni ya Amani Gold Mining walipata leseni kwa kufuata sheria na taratibu zote.

Aidha aliongeza kuwa eneo hilo tayari wao ni wamiliki halali wa leseni na wana sifa zote za kuendeleza shughuli zao za uchimbaji. Alisema tayari ametoa maelekezo kwa wamiliki wa leseni kukaa pamoja na wamiliki wa maduara na kufanya maridhiano na tayari wameanza kulipwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliiambia Nipashe kuwa hayuko tayari kuona wachimbaji hao wanapoteza haki zao na kueleza kuwa tayari ameshazungumza na wachimbaji.

# Wanne mbaroni tuhuma mauaji ya wananchi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kutekeleza mauaji kwa kuwakata mapanga wananchi katika maeneo mbalimbali mkoani humo.

Akithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Leonard Nyandahu, alisema kuwa walifanikiwa kuwakamata baada ya kufanyika kwa msako katika kipindi cha kuanzia Juni 22 hadi Julai 25 mwaka huu.

Kadhalika, alieleza kuwa katika msako huo walifanikiwa kukamata pia vitu mbalimbali vya wizi vilivyoibiwa kwa nyakati tofati mkoani humo.

"Watuhumiwa hawa wanne waliokuwa wakijihusisha na vitendo vya mauaji ya kukodiwa kwa kukata watu mapanga tumewahoji na wamekubali kuhusika na vitendo hivyo katika maeneo mbalimbali," alisema Nyandahu.

Vilevile alieleza kuwa wanaendelea na msako kwa kuhusisha pia mikoa jirani kwa lengo la kukamata mtandao wa wahalifu ambao wanakodiwa.

Pia alieleza kukamatwa kwa bunduki tano pamoja na risasi zaidi ya 300 ambazo zilikuwa zimekodishwa kwenye kampuni za ulinzi kinyume na taratibu, pamoja na waya wa fensi mita 12 mali ya Mgodi wa Buzwagi, mafuta ya dizeli lita 310 pamoja na matairi matano.

Katika hatua nyingine, Kamanda Nyandahu alieleza kukamatwa kwa magari 3,423 na pikipiki 882 kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani, ikiwa ni pamoja na kuzidisha abiria, mwendokasi, kutokuwa na lesseni na madereva 673 walipigwa faini.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi mkoani humo kufuata sheria na taratibu za nchi na kuacha kujihusisha na vitendo vya kiuhalifu pamoja na kuendelea kutoa taarifa za uhalifu kwa Jeshi la Polisi ili wahalifu waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.


# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | JENIFA KALOLI KAPENGA | NYUMBA | ANTHONY LEONARD SANANE | KIPUNGUNI MACHIMBO-ILALA | 10/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SYLIVESTER APOLINARY MBOYA | NYUMBA | SYLIVESTER APOLINARY MBOYA | MBEZI MSUMI | 22/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | DANIELLA'S BRIDAL SOLUTIONS | NYUMBA | ELIJAH SAMSON MWAKILINDI | BUNJU | 10/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | PROTACE GILBERT ZAKE | NYUMBA | PROTACE KATO ZAKE | BOKO DOVYA | 10/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | ZULFA SALIM SALUM | NYUMBA | HILAL MATHIAS MAPUNDA | MAJI MATITU- CHAMAZI | 11/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | HALIMA JUMA HAJI | NYUMBA | HALIMA JUMA HAJI | VIKINDU | 15/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | OBOTTO SILVANUS MAKOSENO | NYUMBA | SILVANUS MAKOSENO | KUNDUCHI MTONGANI | 16/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | REGINA CHARLES KAJOLE | NYUMBA | ATHUMAN RAJABU JONGO | KILUNGULE-MBAGALA | 10/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | SAIDI AKILIMALI KALILWA | MWASONGA-KIGAMBONI | 6/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | MARIAM PATRICK SHAYO | NYUMBA | DORICE YOHANA MWAKAPESA | MBEZI MSAKUZI | 16/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | FRANK SMART MWASHI | NYUMBA | FRANK SMART MWASHI | MAJOHE | 16/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANGWA CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA | JASSON ALPHONCE MWAKITWANGE | BUNJU 'A' | 09/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 10/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ZULFA SHAFII MALENDA | NYUMBA | HALIMA SHAFII MALENDA | NZASA -CHARAMBE | 14/08/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | PRISCUS DIDAS SILAYO | NYUMBA | MOSHI MALINDA | BUNJU "B" | 16/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MAI MEALS LIMITED | NYUMBA | MLIGO MUSSA HAMIS | KIGAMBONI-AMAN GOMVU | 18/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | SALUM RAJABU MCHOMVU | NYUMBA | SALUM RAJABU MCHOMVU | MAJOHE-ILALA | 24/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR.ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI KIPAWA-ILALA | 27/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | MAJOHE-VIWEGE | 27/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMANI OMARI NOMBWANI | NYUMBA | AMANI OMARI NOMBWANI | KIGOGO-KIGAMBONI | 29/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | CESILIA PASCHAL MUSHI | NYUMBA | MAISHA STEVEN MUSHUNGUZI | MABIBO | 22/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | EVODIA ATANAS MBANGALA | NYUMBA | EVODIA ATANAS MBANGALA | UDINDIVU- MAPINGA BAGAMOYO | 17/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SEGUMBA JAPHAR MHANDO | NYUMBA | SEGUMBA JAPHAR MHANDO | VIWEGE MAJOHE | 29/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 23/08/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | RAJABU IBRAHIM MBAMBWA | NYUMBA | RAJABU IBRAHIM MBAMBWA | KIJITONYAMA-ALIMAUA | 17/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 25/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**


1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0787129539/0718038313/0719351040/0785242219/0714939933/0754006181/0759282344
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

ama
ALHAMISI JULAI 27, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Ni maajabu ya papai kwako, kama huli, anza sasa hivi



## Wabunifu UDSM wanapokonga wapishi jikoni, wawaletea 'jikosola'

Ukurasa 12

# Ndiyo ujumbe wa wakulima, wazalishaji mbegu kwa SMZ

• Washangaa mchakato wa sheria unachelewa, wataka ulinzi Vs GMO

**Na Zuwena Shame, aliyekuwa ZANZIBAR**



MBEGU ndiyo mwanzo wa uhai, ni muhimu kwenye kuzalisha chakula, ndiko iliko lishe na maendeleo ya kilimo yanayowapa maisha wengi mijini na vijijini ni chache kati ya sifa nyingi za mbegu.

Bila kuwa na sheria za kulinda na kutunza mazingira ya asili ni vigumu kuwa na mbegu bora zenye ladha na vionjo watu walivyovizoea kwenye matunda, mboga, ndizi, miwa na mahindi.

Ikumbukwe kuwa wakulima ndiyo walinzi wa kwanza wa mbegu, wanazihifadhi na kuzitunza hasa za asili bila malipo, kwa karne nyingi.

Ndiyo maana wakulima na wadau wa kilimo Zanzibar wanaomba serikali yao kuharakisha mchakato wa sheria ya mbegu ili waweze kuzilinda na kutunza mazingira.

Ni ombi linalotolewa wakati wa mkutano wa wakulima wadogo kutoka Bara na Zanzibar, wazalishaji wadogo wa mbegu na asasi za kirai zinazohudumia wakulima.

Wanaamini sheria ni ulinzi wa haki zao kwenye ugunduzi, kutumia, kubadilishana na kuendeleza mbegu za asili.

Mkutano huo unaoandaliwa kwa ushirikiano wa Taasisi za Mtandao wa Vikundi Vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), African Centre for Biodiverity (ACB) na Umoja wa Walima Mboga na Matunda Zanzibar (UWAMWIMA), unahimiza ujio wa sheria hiyo.

Wanasema rasimu ya sheria ya mbegu visiwani haijafika hadharani hivyo kufanya wakulima wadogo kuwa na hofu wa haki zao za msingi katika kulinda na kuziendeleza mbegu zao pamoja na ugunduzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa MVIWATA, Stephen Ruvuga, anasema wakulima wadogo visiwani humo wana hofu ya kupoteza mfumo wao wa kilimo uliopo unaowapa uhuru wa kubadilishana, kuuziana na kupeana mbegu za asili bila mipaka.

Anawaambia washiriki, kuharakisha mchakato wa sheria hiyo ni muhimu kwani Zanzibar ina wakulima wengi wadogo ambao sheria hiyo inawalenga, pia kukamilika kwake kutawawezesha kujua haki zao za msingi ikiwamo kuzihifadhi na kuziendeleza.

Aidha, wakulima wanaitaka SMZ kuiga sheria nzuri za mbegu za mataifa mbalimbali ya Afrika kama Uganda na Ethopia na pia Venezuela huko Amerika Kusini.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) na Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) zinawagusa wakulima, wakizisifia kuwa zimetoa kipaumbele katika kilimo ikolojia na kutambua mbegu za asili zilizopo visiwani humo kwa kuzitafiti.

Ruvuga anaeleza kuwa dhana kuu ya sheria ya mbegu ni kuongoza, kusimamia na kudhibiti biashara yake, hivyo mfumo mbadala ambao sio wa kibishara unatakiwa ili kuzilinda hasa zile za asili ili zisipotee na kwamba ule utamadauni wa kubadilishana mbegu unaheshimiwa, unathaminiwa na kulindwa na ikiwezekana pia miongozo iliyopo itambue.

Mkurugenzi wa Umoja wa Wakulima wa Mboga na Matunda Zanzibar- UWAMWIMA, Khamis Juma, anawataka wajumbe kutumia mkutano huo kujifunza kutoka pande zote mbili za Muungano masuala ya sheria na sera.

Juma anasema: "UWAMWIMA husaidia wakulima kimapato kwa kuuza mazao na mbegu ila sheria na sera zinazomgusa mkulima moja kwa moja zinambana."

"Baadhi ya mbegu zinaingizwa visiwani humo kwa sheria na mamlaka na kusimamiwa pia hivyo kutawala na kuzifunika zile za asili, hata hivyo nyingi hazina ubora zikilinganishwa na mbegu za asili zenye ladha halisi."

Mwanaharakati wa kilimo hai - Zanzibar, Mwatima Juma, anasema mbegu ni suala pana hivyo kuweka sheria ngumu kunaweza kuwaathiri wakulima hasa wadogo kwani mbegu ni biashara, akionya kuwa wakulima wengi visiwani humo hawajafikia kuwa na upeo wa kuzalisha kibiashara.

Anatoa mfano kuwa si vyema sheria hiyo itakayotungwa kuwa na ajenda za nje mfano mbegu za mkulima lazima ziwe na lebo na kuthibitishwa ili iwe ya kibiashara kwani wakulima wengi wadogo wamezoea kupeana na kubadilishana mbegu wenyewe kwa wenyewe.

"Sheria ya mbegu isiwe kwa wote (uniform) na kuwabana wakulima wadogo. Ilenge zaidi katika makampuni yanayotuletea kutoka nje tena ambazo si bora na hazijakubaliwa na taifa kama zilizobadilishwa nasaba za GMO." anasema Mwatima.

Asia Thani, kutoka Wizara Ya Kilimo Zanzibar anaelezea suala la

Inaendelea Uk. 14

MAZINGIRA

# Wabunifu UDSM wanapokonga wapishi jikoni, wawaletea 'jikosola'

Na Christina Mwakangale

MATUMIZI ya nishati ya kupikia hayaepukiki, yanahitajika kila siku, haijalishi ni umeme, mkaa, kuni au gesi cha msingi ni mlo uandaliwe na familia ikutane mezani, asubuhi mchana na jioni.

Lakini, tatizo ni nishati inayofaa kutumiwa tena yenye gharama nafuu. Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira, linakadiria kuwa zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania hutumia nishati isiyo salama kama mkaa, mafuta ya taa au kuni kupikia.

Ni nishati hizo zinaelezwa kuwa huzalisha kaboni au hewa ukaa nyeusi, mojawapo ya gesi zinazochangia mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la joto duniani, yote yakiidhuru dunia.

Katika maeneo mengine wanavijiji hutegemea samadi ya mifugo kupikia baadhi wakitumia mabaki ya mazao kama makumbi ya nazi, maganda ya mihogo na mabua ya mahindi jikoni.

Katika juhudi za kupata nishati safi na salama jikoni kuna mipango mingi kuanzia, kutumia majiko banifu ya umeme, mkaa na kuni, gesi asilia na hata mkaa mbadala.

Wasomi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Daud Nzunda na Laetus Buberwa, wanashirikiana, kwenye ubunifu unaoleta jiko bora kupunguza gharama za nishati ya kupikia. Tena pia wakisaidia teknolojia inayolinda afya na mazingira.

Watafiti hao wamebuni jiko la sola linaloakisi mwanga wa jua kisha sufuria kubandikwa kwenye mfumo ulioundwa maalum kuivisha chakula.

Wawili hao ni wanafunzi walio chini ya kiatamizi cha kukuza bunifu cha UDSM, wanaeleza kazi yao kwenye maonesho ya Sabasaba wakizungumza na Nipashe na kufafanua kuhusu jiko hilo la sola.

Daud anasema mfumo huo, ambao unatumia mionzi ya jua kupata nishati ni mahususi kwa ajili ya kupikia na kwamba limetengenezwa kwa vifaa vya bati la aluminiam vinavyoakisi mwanga na kukusanya mionzi.

Ndiyo inayosababisha chuma kilichowekwa katikati ya aluminum hiyo kupata moto na kuivisha vyakula kuanzia makande na maharagwe kwa gharama nafuu.

"Mfumo huo wa kutumia vifaa vya aluminiam ambavyo vinaukusanya mwanga wa jua halafu vinauelekeza sehemu moja ambayo ina sufuria kisha inaufyonza na kutengeneza joto kali linalotumika kupikia vyakula mbalimbali," anaongeza.

"Ni mfumo unaoweza kutumika vijijini na kuondoa ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa, unaweza ukafanya kazi vizuri ya kupika vitu mbalimbali kuanzia chakula vya aina zote wakati jua likiwaka vizuri unaweza kutumia saa moja tu ukaivisha hata vyakula vigumu kama maharage," anasema Daud.

Msomi huyo anasema muundo wa jiko hilo utategemeana na ukubwa sufuria, na iwapo familia ina watu wengi litaundwa kubwa zaidi ili kukidhi mahitaji ya watumiaji hao.

"Limetengenezwa maalum kwa watu wa hali ya chini maana hata gharama yake siyo kubwa. Mteja yeyote anauwezo wa kulimudu na uzuri ukishakuwa nalo, hauitaji gesi au mkaa. Huna sababu ya kuhangaika kutafuta nishati nyingine jua linatosha," anasema msomi huyo.

Kuhusu gharama, Daud anasema likishatengenezwa, bei ni kuanzia Shilingi 100,000 kutegemeana na uwezo ama ukubwa wa chombo.

"Hilo jiko ni zuri na ukishakuwa nalo ni jumla hamna haja ya kwenda kununua mengine. Pia kama mtu wa kawaida ana vyanzo vingine vya nishati anaweza akalitumia, kuivisha vyakula vya muda mrefu mfano maharagwe.

"Linapunguza gharama kwa sababu vyakula vinavyoiva kwa muda mrefu badala ya kuvipika kwenye gesi au mkaa au jiko la umeme, unaweza ukaamua kuvipika kwenye jua kupitia jiko hili.Halafu vile vinavyoiva muda mchache upikie katika nishati nyingine," anashauri.



Mgunduzi Daud Nzunda, akielezea ufanisi wa jiko linalotumia mwanga jua linaloundwa na mabati ya aluminiam ambayo hukusanya miale na mionzi katikati na kuiakisi kwenye sufuria ili kuivisha chakula kutokana na nishati ya sola: **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

> "Mfumo huo wa kutumia vifaa vya aluminiam ambavyo vinaukusanya mwanga wa jua halafu vinauelekeza sehemu moja ambayo ina sufuria kisha inaufyonza na kutengeneza joto kali linalotumika kupikia vyakula mbalimbali," anaongeza.

**LINAKAA NJE**

"Ni vizuri zaidi uliweke nje kwa kuwa kuna mwanga wa jua wa kutosha na inakuwa rahisi zaidi na kwa haraka zaidi ukitumia muda mfupi," anaongeza Daudi.

Anasema linaweza kudumu kwa miaka mitano hadi 10 na kwamba matumizi yake hayasumbui cha msingi ni kuwekwa kwenye jua la kutosha hasa nje.

Anaongeza kuwa majiko hayo hayajaanza kuuza rasmi lakini kwa mtu anayehitaji anaweza akatoa oda akaletewa maana ni teknolojia ambayo kila kitu kimekwishafanyiwa uchunguzi na utafiti wa kutosha.

"Jiko likiwa pana zaidi, unaweza kubandika sufuria ambayo ina ukubwa kulingana na sehemu iliyotengenezwa kuhifadhi mwanga. Tumeongeza ukubwa, ili iweze kufanya vitu vingi zaidi lakini ukitaka ndogo zaidi ya hii nayo inapatikana."

Ingawa wanaharakati wa mazingira duniani hivi sasa wito wao ni ulinzi wa bayoanuai na na mifumo ya ikolojia, suala la kupata nishati mbadala nalo halikwepeki kwa vile ndiyo msingi wa dunia endelevu.

**NIA YA SERIKALI**

Nia ya serikali ni kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2033, ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, anaongeza zaidi kuwa mbadiliko ni lazima kwa vile ni asilimia nane pekee ya Watanzania takribani watu milioni 7.5, ndiyo wanaotumia nishati safi.

Na kwamba azma ya serikali ni ndani ya miaka 10 asilimia 80 ya wananchi iwe inatumie nishati safi kupikia iwe nyumbani, vyuoni na kwenye taasisi za umma za huduma.

Dar es Salaam ndilo jiji kubwa la kibiashara ambalo linaelezwa kutumia zaidi ya asilimia 50 ya mkaa unaozalishwa nchini.

Ni kwa mujibu wa mdau wa nishati safi, Leonard Kushoka, mzalishaji wa mashine za kutengeneza mkaa mbadala huko mkoani Tabora, anayesema amefanya utafiti kubaini hayo.

AFYA

# Mmomonyoko maadili unapoelekea kuwa adui namba 4 wa maendeleo

## • Ulikuwa ujinga, umaskini lakini sasa…



Katibu Mkuu, Dk. John Jingu, akizungumza na washiriki kuhusu mmomonyoko wa maadili.

**Na Sabato Kasika**

TANZANIA ilipambana na madui watatu ujinga, umaskini na maradhi lakini zama hizi kuna uwezekano wa kuongezeka mwingine, naye ni mmomonyoko wa maadili.

Adui huyo anachangia kwa kiasi kikubwa unyanyasaji wa kijinsia, huathiri afya kimwili akili na anaweza kusababisha kujidhuru, kujitenga, kukata tamaa na hata kujiua.

Miongoni mwa matatizo yanayoikabili jamii inayotajwa kusababisha kuwapo kwa watu wenye matatizo ya afya ya akili, watoto wa mitaani, matumizi ya dawa za kulevya, ubakaji, kujitia kitanzi, ulawiti, ushoga na usagaji ni mmomonyoko wa maadili.

Ni suala linaloigusa serikali kutafuta ufumbuzi, hivyo kutokana na kuendelea kuwapo kwa mwenendo huo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na viongozi wengine wanajichimbia ndani kwa siku kadhaa kuweka mikakati ya kumshinda adui huyo wa taifa.

Ni katika kusanyiko la viongozi wa dini kuhusu wajibu wa wazazi na walezi, katika malezi na familia linalokutana hivi karibu , Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. John Jingu, akisema migogoro ya kifamilia inachangia watoto kuwa katika hali mbaya ya malezi na kuongezeka ukatili dhidi yao.

Akitoa maelezo yake kwa viongozi hao, Dk. Jingu anasema hadi kufikia Machi mwaka huu, watoto 335,971, walikuwa wakiishi katika mazingira hatarishi na kufanya kazi mtaani, kitendo ambacho ni hatari kiafya.

"Takwimu za Jeshi la Polisi kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2022, zinaonyesha kuwa kulikuwa na matukio 12,163, huku ya ubakaji ni 6,335, ulawiti ni 1,557 na mimba za utotoni ni 1,555," anasema Dk. Jingu.

Anasema jumla ya watoto 2,185 kati yao wa kiume 1,324 na wa kike 861 waliokuwa wanafanya kazi na kuishi mitaani waliunganishwa na familia zao ili kuwasaidia watoto hao na kwamba serikali imeratibu uanzishwaji wa makao ya watoto 333 ya serikali na binafsi ambayo yanahifadhi watoto 12,077.

"Hali hii siyo nzuri, ndio maana tumewaita ili kuweka mikakati kwa pamoja kwa lengo la kuwalinda watoto kuanzia kwenye malezi hadi kwenye afya zao, kwani mazingira ya mitaani si salama kiafya, wanaweza kukumbukwa na magonjwa mbalimbali ukiwamo UKIMWI," anasema.

**USHIRIKIANO VITANI**

Katibu anawataka viongozi wa dini kushirikiana na serikali katika vita dhidi ya mmomonyoko wa maadili, kwa kuwa wao wana nafasi kubwa ya kutoa elimu kupitia nyumba za ibada.

"Vita hii ni yetu sote nyie viongozi wa dini ni muhimu kushiriki kikamilifu kuelimisha jamii kutambua umuhimu wa maadili mema ili kuepusha vitendo vya ukatili, ambavyo vinahatarisha usalama watoto," anasema.

Anabainisha kuwa mmomonyoko huo wa maadili, imeifanya serikali kuandaa mwongozo unaoelekeza namna bora ya malezi ya watoto na familia kwa kuzingatia mazingira na kwamba unasisitiza zaidi wajibu wa wazazi au walezi katika malezi ya watoto na familia.

"Mwongozo huo wa kitaifa unajulikana kama 'Familia Bora, Taifa Imara' Mwongozo wa Taifa wa Wajibu wa Wazazi na Walezi katika Malezi ya Watoto na Familia wa mwaka 2023," anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Jingu, lengo lake ni kujengeana uelewa na uzingatiaji wa masuala ya msingi kama taifa kuhusu wajibu wa wazazi au walezi kwenye malezi ya watoto na familia.

**HALI NI MBAYA**

Mwenyekiti Mwenza wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) Askofu Dk. Stanley Hotay, akitoa mchango wake, anasema hali ya maadili ni mbaya hasa kwa wa watoto wa kiume ambao wamekumbwa na ushoga.

Kiongozi huyo anasema katika jamii, mtoto wa kiume amesahauliwa, huku hali yake ikiendelea kuwa mbaya kwenye maandalizi ya kuwa baba wa familia na kwamba watu waunge mkono serikali kuimarisha maadili.

"Wanapewa kipaumbele watoto wa kike kuwa wanafanyiwa ukatili lakini wa kiume nao wanafanyiwa ukatili kupitia wa ulawiti na kuwa mashoga huko wanakokimbilia baada ya kufika nyumbani kwao," anasema Askofu Hotay.

Anasikitishwa na janga la watoto wa mitaani, akisema hao sio yatima bali wana wazazi, ila migogoro ya familia, ugumu wa maisha, matumizi ya dawa za kulevya na vingine vingi, vinachangia kuwakimbiza kwenda kuishi huko.

"Hebu tufikie kuwa kama wazazi wetu wangetulea vibaya leo tungekuwa hapa? Viongozi wa dini tunaahidi kutoa ushirikiano kwa serikali katika vita hii ya kutaka kumaliza tatizo na kulinda afya za vijana hao wadogo," anasema.

Mwakilishi wa Mufti wa Tanzania, Sheikh Ally Nguruko, anasema Mufti Seikh Dk. Abubakar Zubeir Bin Ally, ameandika kitabu kinachozungumzia malezi bora, na kwamba hivi karibuni kitakuwa kimetoka.

Aidha, anasema wazazi na walezi hawawezi kukwepa kusimamia malezi kwa watoto wao na kufanua kuwa ni wajibu wao kuhakikisha wanawaandaa vizuri watoto wao, kwa kuwa ndio taifa la baadaye.

Sheikh Nguruko anasema wazazi na walezi wapoacha kutimiza wajibu wa kusimamia malezi bora, matokeo yake ni mmomonyoko wa maadili ambao unaikabili jamii kwa sasa ikiwamo vitendo vya ushoga.

"Lakini tusiishie katika warsha na makongamano, bali vikao hivi vije na matokeo mazuri ya kufanikisha vita dhidi ya mmomonyoko wa maadili, kwani vijana na jamii kwa ujumla imeharibika," anasema Sheikh Nguruko.

Aidha, anaishukuru serikali kwa kutambua mchango wa viongozi wa dini na kuwashirikisha wenye suala hili la kujadili mmomonyoko wa maadili ndani na jamii na kuahidi kushirikiana na serikali ili kumaliza tatizo hilo.



Baadhi ya viongozi wa dini wakishiriki mkutano wa kutafuta mikakati ya kunusuru maadili. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

AFYA

# Ni maajabu ya papai kwako, kama huli, anza sasa hivi



**Na Mwandishi Wetu**

KULA papai ni jambo jema na hizi ni faida za kushangaza ambazo pengine hukuzijua unapotumia tunda hilo, unaweza kuzipata.

Kwa mujibu wa BBC, papai ni tunda la kushangaza na lenye afya. Ina 'antioxidants' ambayo hupunguza kuvimba na kupambana na magonjwa na kusaidia mtu kuonekana na umri mdogo. Kwa hiyo badala ya kukimbilia vidonge vya kuondoa makunyanzi usoni na ngozi kukakamaa ukila papai ni dawa.

**HUZUIA SARATANI**

Kwanza lina virutubisho tele kuanzia kalorisi (kupata nguvu), lina wanga, limejaa nyuzi nyuzi hivyo huwezesha chakula kutembea haraka tumboni na kupunguza kupata haja ngumu, limesheheni protini, vitamini C, A, B9, madini ya potasiamu, kalshamu na magnesiamu.

Kikubwa zaidi linatajwa kuwa huzuia saratani. BBC inasema utafiti unaonyesha kuwa 'lycopene' iliyomo kwenye papai inaweza kupunguza hatari ya saratani. Inatajwa kuwa ni muhimu kwa watu wanaopata matibabu ya saratani.

Papai lina wingi wa vitu vya kuzuia saratani ikiwa ni pamoja na folate, vitamini C, beta-carotene na vitamini E ambayo hupunguza hatari ya saratani mwilini.

Utafiti mdogo uliofanywa kwa watu wazima wenye kuvimba na shida ya tumbo, ulipunguza madhara ya msongo na seli za saratani. Hata hivyo, utafiti zaidi unahitajika kabla ya kufikia hitimisho.

**KUPUNGUZA LEHEMU**

Cholesterol au lehemu na afya ya moyo ni tatizo linalofumbuliwa na papai. Utafiti unaonyesha kuwa matunda na mboga zenye 'lycopene na vitamin C zinaweza kuzuia magonjwa ya moyo. Antioxidants zinazopatikana kwenye papai hulinda mishipa ya moyo dhidi ya kuzibwa na cholesterol au lehemu na kusababisha mshtuko wa moyo na hata kifo.

**HUONDOA GESI**

Linapokuja suala la gesi na ukosefu wa chakula tumboni papai ni jibu. Hupunguza asidi tumboni, ikiwa mtu ana kiungulia na maumivu ya tumbo, papai ni tiba. Papai pia ni tiba ya shida ya kukosa kusaga chakula au colic.

Kwa upande wa afya ya ngozi na nywele, papai hung'arisha ngozi na kukuza nywele kutokana na wingi wa vitamin A iliyomo na kuamsha tezi za mafuta mwilini na nywele. Pia papai hupunguza chunusi ndio maana baadhi ya kampuni hupendekeza soko la mfuta 'krimu' au losheni za ngozi zao ambazo zimetengenezwa au zenye papai.

Maumivu ya hedhi yanadhibitiwa na papai kwani ni miongoni mwa vyakula vinavyotumika kwa maumivu wakati wa hedhi, kwa vile papai huwa na kitu kinachojulikana kwa jina la "papain" ambacho kinahusiana na damu ya hedhi. Imeonekana kuchangia katika kurekebisha na kuboresha hali hiyo.

**KULINDA JICHO**

Mtoto wa jicho anaweza kukabiliwa na papai imebainika kuwa hupunguza hatari ya mtoto wa jicho. Papai lina wingi wa vitamin A na beta-carotene ambazo ni muhimu kwa afya ya macho na uwezo wa kuona. Papai na karoti ni vyakula viwili ambavyo vimekubaliwa kuyapa macho afya kamili.

Lakini kwa upande wa asma au pumu, papai ni moja ya vyakula vinavyopunguza hatari ya pumu kwa sababu lina beta-carotene nyingi. Ikiwa una pumu, jaribu kula papai.

Afya ya mifupa nayo inaongezeka kwa vile huongeza ufyonzaji wa kalsiamu kutoka kwenye mifupa, hupunguza utolewaji wa kalsiamu na figo, na huwa na protini zinazolinda mifupa, ambazo zote kwa pamoja husababisha mifupa yenye afya, inasema BBC.

**KWAKO MSOMAJI**

Angalizo hili siyo sehemu ya makala ya BBC, kwa ujumla papai ni mmea rahisi kuotesha kwenye udongo wowote ambao hautuami maji na usio oevu (majimaji). Mti na matunda yake huhitaji kiasi kidogo cha mvua. Hivyo jitahidi kuupanda wakati majira ya masika. Kuwa na miche kadhaa nyumbani kwako.

Baridi kali au joto kali linaweza kudhuru mti na matunda yake, hivyo kama kuna baridi sana huna haja ya kupanda tunda hili. Miti ya mipapai na matunda yake hustawi katika halijoto ya kuanzia nyuzi joto 21 hadi 32 ndiyo maana karibu kila nyumba mijini inaweza kustawisha mapapai.

Hali ya hewa kavu huongeza ladha ya matunda wakati wa kukomaa ndiyo maana wakazi wa Dar es Salaam na miji mingine yenye joto kama Mwanza, Musoma, Dodoma na Morogoro wanafurahi utamu wa tunda hilo.

Zaidi ya hayo, inaweza kuchukua muda wa miezi 8 hadi 10 kwa mbegu za mipapai kuzaa matunda baada ya kupandwa, kutegemeana na hali ya mazingira, mti wa papai unaweza kutoa matunda 30-150 kwa mwaka, kwanini usipande na kuwa tajiri wa matunda?

## NDIYO UJUMBE WA WAKULIMA, WAZALISHAJI MBEGU KWA SMZ

Inatoka Uk. 11

kuchelewa kwa sheria hiyo kuwa kunafanya wafanyabiashara wengi kuingiza kila aina ya mbegu visiwani humo na kufanya kama dampo la kuzitupia.

"Kila mtu anaingiza mbegu zake ambazo hazina sifa wala ubora kwani baadhi hazioti na zimechanganyika na hakuna sheria wala chombo cha kuwashtaki, shida zote hizi zitaondoka kwa sababu kutakuwa na mamlaka ya kusimamia sheria za mbegu," anasema Asia.

Ofisa Tafiti na Utetezi kutoka Shirika la African Centre for Biodiversity (ACB), Sabrina Masinjila, anaueleza mkutano kuwa sheria ya mbegu visiwani humo ni lazima kuangalia baadhi ya mikataba ya kimataifa mfano International Union for the Protection of New Varities of Plants (UPOV).

Mkataba huo moja ya sheria zake hazimruhusu mkulima au mtu kutumia mbegu kijamii kitu ambacho wakulima wengi wameshazoea kwa kubadilishana na kupeana bila mipaka.

Anaeleza kuwa UPOV isiwe ni kipimo cha kuendeleza kilimo kwa nchi kama Tanzania kwani kiuhalisia Zanzibar, Tanzania Bara na nchi nyingine nyingi bado hazijafikia malengo wala mahitaji hayo.

Anasema rasimu hiyo inapaswa kukwepa mapungufu ya wazi ikiwamo kutohusisha baadhi ya vifungu katika sheria ya mbegu ya Tanzania Bara ya mwaka 2003 ambavyo vimeshindwa kutoa ulinzi kwa wakulima wadogo ili wawe wanauziana na kubadilishana mbegu zao kwa uhuru.

Mkuu wa Program kutoka MVIWATA, Theodora Pius, anasema ni wakati muafaka kuwatambua wazalishaji mbegu zinazotumika katika kuzalisha chakula.

Theodora anasema kuwa MVIWATA hasa mkoa wa Dodoma wameweza kuendesha programu kubwa kwa wakulima wa mbegu ili waweze kuzalisha mbegu za asili katika vikundi, lakini baadhi ya wazalishaji wakubwa wamekuwa wakiwalaghai kwa kununua mbegu na kuziwekea vibandiko vyao ili zionekane kuwa wao ndiyo wazalishaji.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Seif Mwinyi anawaambia washiriki kuwa serikali imechukua mapendekezo yaliotolewa na wadau hao hasa ikiwamo mfano wa sheria ya mbegu ya nchi za nje ambazo hutambua haki za mkulima na kuthamini mbegu za asili.

"Rasimu ya sheria imejikita sana katika kuongeza uzalishaji, ajira kwa vijana na akina mama na masoko na kutanua wigo wa bidhaa zetu. Tumeona kwamba ili kuwe na uzalishaji mbegu ndiyo msingi mkubwa," anasema Mwinyi.



## 'Wasauzi' waja Tanzania kujifunza ufugaji nyuki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imepokea ugeni wa watu 10 kutoka nchi ya Afrika Kusini waliokuja kujifunza juu ya ufugaji nyuki, hasa kwenye maeneo ya uanzishaji wa manzuki (mizinga ya nyuki) na hifadhi za nyuki.

Ugeni huo uliwasili juzi jijini hapa ukijumuisha wataalamu na wafugaji nyuki ambapo malengo yao ni kujifunza kuhusu maandalizi na ukaguzi wa manzuki pamoja na njia bora za kuzuia na kudhibiti wadudu kwenye ufugaji nyuki.

Akiongea baada ya wageni hao kuwasili, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamishna Benedict Wakulyamba, alisema ziara hiyo ni ya kimkakati na inalenga kuanzisha mazungumzo na kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika Kusini, husus katika eneo la biashara ya mazao ya nyuki, teknolojia za ufugaji nyuki na utafiti.

Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, kutoka Wizara ya Maliasili na Utali, Deusdedith Bwoyo, alisema wageni hao wamehamasika kuja hapa nchini kujifunza namna shughuli za ufugaji nyuki zinavyofanyika.

"Kule Afrika Kusini tumeambiwa wana uwezo wa kuzalisha tani 2,000 kwa mwaka wakati asali inayohitajika ni tani 4,000 kwa mwaka, sisi huku tuzalisha tani 32,691 kwa mwaka na tunatumia asali hiyo ndani ya nchi karibia asilimia 90," alisema Bwoyo.

Pamoja na hayo, Bwoyo alisema wageni hao wamekuja kujifunza namna bora ambayo itawasaidia kuongeza uzalishaji wa asali nchini kwao, lakini pia namna ambavyo wanaweza kuwahamasisha watu nchini kwao kutumia asali kwa wingi kama ambavyo zao hilo la nyuki linatumiwa kwa wingi hapa nchini.

Kiongozi wa wajumbe hao ambaye ni Mkuu wa Idara ya Kilimo na Maendeleo Vijijini Kaskazini Magharibi mwa Afrika Kusini, Zakaria Thupi Mokgathlha, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye eneo la ufugaji nyuki, hivyo wamekuja kujifunza ili waweze kupata ujuzi utakaowasaidia kujiimarisha kwenye eneo hilo.

"Tumekuja kuangalia Tanzania inavyofanya kwenye eneo hili ili tutakavyorudi kwetu tukaweke mikakati ya kuimarisha sekta hii." Alisema Zakaria.

Baada ya kuwasili jijini Dodoma, ugeni huo ulipata fursa ya kutembelea ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wilayani Manyoni pamoja na Hifadhi ya Nyuki ya Agondi.

# Wananchi walalamika kupewa furushi la dawa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WANANCHI wa Kitongoji cha Majengo Kata ya Manyoni mkoani Singida wamewalalamikia madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni kwamba wamekuwa na tabia ya kuwapa dawa nyingi zikiwamo hata ambazo hazihitajiki wanapokwenda kutibiwa katika hospitali hiyo.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, wakati wa mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi ikiwa ni utaratibu aliojiwekea kila mwezi kusikiliza kero kila wilaya ili kuzipatia ufumbuzi.

"Katika hospitali yetu ni majengo tu ndiyo yapo hakuna huduma bora ukienda kutibiwa unaandikiwa rundo la dawa kama vile wanakukomoa na nyingine zinakuwa wala hazihitajiki tunaomba mtupie macho katika hospitali hiyo," alisema Ezekiel Jonas.

Jonas alisema hata wazee wanatozwa fedha wanapokwenda kutibiwa na kumuomba Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemilembe Lwota, awe anafanya ziara ya kushtukiza katika hospitali hiyo hata mara moja kwa wiki ili ajionee mambo ya ovyo yanayofanyika katika hospitali hiyo.

Mwananchi mwingine, Biswahillah alisema pamoja na kwamba serikali ikishatoa mwongozo kwa watoto wadogo wenye chini ya miaka mitano wasitozwe fedha wanapokwenda kutibiwa lakini katika hospitali hiyo hali ni tofauti wanatozwa fedha.

Malalamiko mengine yaliyotolewa na wananchi ni kwa Jeshi la Polisi Wilaya ya Manyoni ambapo walisema wakienda kwenye kituo cha polisi kuomba kumwekea dhamana mtu wanalazimishwa kutoa rushwa.

Wananchi hao pia walilalamikia maofisa maliasili kwa kushindwa kuwasaidia kudhibiti tembo ambao wamekuwa tishio kutokana na kuharibu mazao yao shambani na kuua watu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alijibu malalamiko hayo alimwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Furaha Mwakafwila, kufanya uchunguzi suala wagongwa kupewa dawa nyingi.




Kaimu Mkurugenzi wa Elimu Maalum Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), George Mbijima (wa nne kulia), akikabidhi pikipiki kwa Philip Mahula wa Shule ya Msingi Mwitikira, wilayani Bahi, aliyewawakilisha walimu kutoka mikoa ya Dodoma na Morogoro zilizotolewa jana na Mradi wa Elimu Jumuishi na Ufundishaji Tembezi kwa watoto wenye changamoto ya macho unaosimamiwa na mradi wa Shirika la Light for the World Tanzania kwa ajili ya kuwawezesha walimu wa elimu maalum kutimiza majukumu yao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Polisi yawashukia madereva wanaoendesha kwa mazoea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limewataka madereva kuacha tabia ya kuendesha magari kwa mazoea, badala yake wachukue tahadhari ili kuepusha ajali za kizembe ambazo zimekuwa zikiwahusisha watembea kwa miguu barabarani.

Aidha, jeshi hilo limezishauri klabu ambazo zinafanya mazoezi pembezoni mwa barabara kutumia upande wa kulia, ili kuona gari linalokuja mbele yao ikiwa ni pamoja na kutumia mistari mitatu badala ya kusambaa barabarani wakati wa mazoezi hayo.

Kauli hiyo imetolewa na Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, baada ya kutokea kwa ajali iliyohusisha klabu ya jogging ya jijini Mwanza kugongwa na kusababisha vifo vya watu sita waliokuwa katika mazoezi.

Kamanda Misime alisema madereva wengi wamekuwa na tabia ya kuhisi aliyembele yake au pembeni yake anamuona kitu ambacho katika udereva hakipo bali wanatakiwa kuwa makini na kuchukua tahadhari wakati wowote hata kama wapo ndani ya sheria.

"Madereva mnapaswa kuondoa kauli au hisia ya kwamba mtu wa pembeni yako, au mbele yako anakuona, mkifanya hivyo mtasaidia kupunguza ajali barabarani," alisema Kamanda Misime.

Aidha, alizishauri klabu za jogging kuacha kusambaa barabarani wakati wa kufanya mazoezi, badala yake watengeneze mistari mitatu ikiwamo kubana pembeni mwa barabara.

Misime alisema wakifanya hivyo kutazisaidia klabu hizo kuwa katika hali ya usalama kwa kutumia eneo dogo tofauti na kuweka mistari mingi ambayo inaweza kusababisha ajali.

Kadhalika, alisema dereva yoyote atakayebainika kukiuka sheria za barabarani Jeshi la Polisi litachukua hatua kali dhidi yake ili iwe fundisho kwa wengine wanaodharau alama za barabarani pamoja na sheria za usalama wa barabarani.

"Madereva mnapaswa kuzingatia sheria za barabarani na hilo sio ombi ni amri na inapaswa kutekelezwa ili kusaidia kuepusha ajali za barabarani za watembea kwa miguu na baina ya magari yenyewe," alisema Misime.

Wakati huo huo Kamanda Misime alisema Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na sheria za usalama barabarani ili kusaidia kuepusha ajali ambazo zinaweza kuepukika.

Alisema elimu hiyo wamekuwa wakitoa katika maeneo mbalimbali huku akisisitiza jamii izingatie sheria za barabarani zinazofundishwa na jeshi hilo.



# CCM yanusa ufisadi ujenzi machinjio, yatoa maagizo kwa RC

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imenusa ufisadi kwenye mradi wa ujenzi wa jengo la machinjio ya kisasa ya Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambayo imejengwa kwa Sh. milioni 150.

Aidha, kamati hiyo imetoa siku 14 kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, kutumia vyombo vyake kuchunguza mradi huo.

Hayo yalibainika juzi wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kukagua mradi huo ambapo ilisema jengo hilo haliendani na thamani ya fedha zilizotajwa kutumika. Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo, alisema pamoja na maagizo hayo pia atawasiliana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

Alisema halmashauri hiyo imeomba zaidi ya Sh. milioni 980 kutoka serikali kuu kwa ajili ya kuweka vifaa vya kuchinjia lakini serikali inasita kutoa fedha hizo kwa sababu jengo limejengwa chini ya kiwango.

"Hatujaridhishwa kabisa na mradi huu, tunamkabidhi Mkuu wa Wilaya achukuwe hatua za haraka kuchunguza akitumia vyombo vyake, wakati huo tunamwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri kulikarabati jengo hili ili liendane na machinjio ya kisasa," alisema Dk. Mwakajumilo.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela aliwataka wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuilinda miundombinu ya machinjio hiyo pamoja na vifaa.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuna tatizo la usimamizi wa miradi hali ambayo ndiyo inayosababisha kutekelezwa chini ya kiwango na hivyo kutowanufaisha wananchi ipasavyo.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda, alisema jengo la machinjio hiyo lilijengwa kwa kutumia akaunti ya dharura ambapo lilijengwa na mafundi wa mtaani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba, alisema atashirikiana na wataalamu wa halmashauri hiyo kutekeleza maagizo ya kamati ya siasa.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, akizungumza na wakazi wa Kata ya Nsalala katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi jana, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya chama hicho ya kukagua miradi ya maendeleo ikiwamo soko ambalo limekwama kuanza kutumika kwa muda mrefu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kikongwe aomba msaada matibabu ya nyonga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MZEE mmoja aitwaye Michael Mwaipopo (65) Mkazi wa Kijiji la Ibanga kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, amekaa ndani kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kupata matibabu baada ya kuteguka nyonga kutokana na kukosa fedha.

Mzee huyo amewaomba Watanzania wenye uwezo kumsaidia kupata matibabu ili arejee katika hali yake ya awali kwa maelezo kuwa kwa sasa hawezi kufanya shughuli yoyote ya kuzalisha kutokana na kushindwa kutembea.

Akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake juzi, Mwaipopo alisema alipata ajali mwaka mmoja na miezi sita iliyopita na akateguka kiuno na nyonga na hakuwahi kupata matibabu kutokana na hali ngumu ya kiuchumi.

Alisema aliamini kwamba angepona bila kwenda hospitalini lakini kwa sasa amebaini kuwa hali yake inazidi kuwa mbaya kutokana na maumivu kuongezeka huku akiwa hana fedha za kumsaidia kutibiwa.

"Nawaomba Watanzania wenzangu wenye uwezo wanisaidie michango ili niende hospitalini nikatibiwe, nimeteseka kwa muda mrefu na sina msaada wowote," alisema Mwaipopo.

Alisema kabla hajapata ajali hiyo alikuwa anajishughulisha na kilimo na kwamba hata siku aliyoanguka alikuwa anatoka shambani na kwamba kwa sasa hawezi kuzalisha tena na hana fedha za kuajiri vibarua.

Mwaipopo alisema kwa muda wote amekuwa akisaidiwa na majirani zake ambao alidai kuwa na wenyewe wana shughuli za kufanya na hivyo huwa anabaki peke yake bila msaada wakiwa kwenye shughuli zao hasa za kilimo.

# OTTU yaandaa mtaala utakaowahusu wafanyakazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO cha Wafanyakazi Tanzania (OTTU) kilichopo jijini Mbeya, kimeanza kuandaa mtaala mpya wa masomo ambao utawafanya wafanyakazi wa kada mbalimbali kusoma kozi za muda mrefu na kuwaongezea zaidi maarifa.

Mkuu wa chuo hicho, Hezron Kaaya, alisema kwa sasa wanatoa kozi za muda mfupi ambazo huwa hazizidi miezi sita jambo ambalo wamebaini kuwa linahitaji kuboreshwa ili kuwaongezea zaidi maarifa wafanyakazi.

Alisema kwa sasa wanakusudia kuanza kutoa kozi ya mwaka mmoja ambayo itawafanya wanafunzi kusoma vitu vingi zaidi na kuboresha utendaji kazi wao kwenye vituo vyao vya kazi na kuboresha tija.

Mmoja wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi ya chuo hicho, Joseph Sayo, alisema kikao walichofanya juzi kilikuwa cha kwanza cha utendaji ambacho ndicho kinaanza mchakato wa maboresho.

Alisema katika kikao hicho walijadiliana mambo mbalimbali ikiwamo uboreshaji huo wa mitaala ili kuendana na mazingira ya sasa pamoja na mahitaji ya wanafunzi ambao wanasoma chuoni hapo.

Mwenyekiti wa bodi ya chuo hicho, Tamimu Salehe, alisema kozi zinazotakiwa kutolewa chuoni hapo zinamahitaji makubwa kazini na hivyo watahakikisha wanafanikisha kusajili na kuanza kuzifundisha.

Mwakilishi wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Mahija Waziri, aliutaka uongozi wa chuo hicho kuandaa mtaala ambao unaendana na vigezo vilivyowekwa na baraza hilo.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alishauri uongozi wa chuo hicho kuangalia namna ya kutoa mafunzo pia kwa wafanyakazi wa sekta zisizokuwa rasmi.

Alisema kwa sasa chuo hicho kinaonekana kama ni cha wafanyakazi wa serikali pekee na hivyo kuwafanya wafanyakazi wa sekta binafsi kutokithamini.



# Lishe duni chanzo wajawazito kufariki wakijifungua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LISHE duni kwa wajawazito imetajwa kuwa ni miongoni mwa sababu ya kuongezeka kwa vifo vya mama vitokanavyo na uzazi kabla au baada ya kujifungua.

Hayo yameelezwa na mtaalamu wa maradhi ya kinamama na uzazi, Dk. Ummulkulthum Omar wakati akitoa mafunzo ya afya ya uzazi kwa waandishi wa habari.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) ofisi ya Zanzibar yalifanyika katika ofisi za chama hicho, Tunguu Zanzibar.

Alisema lishe duni kwa wajawazito husababisha upungufu wa damu mwilini na kuna uwezekano mkubwa wa kupata matatizo wakati wa kujifungua au baada ya kujifungua.

Alisema asilimia kubwa ya wajawazito wanaofika katika hospitali kujifungua huwa na upungufu wa damu jambo ambalo ni hatari kwa afya ya mama na mtoto.

"Baadhi ya wanawake wanapokuwa na ujauzito wanapenda kula vyakula vya onyo ambavyo havina faida katika kuimarisha afya zao......utakuta anakula udongo au mkaa kwanini wasile vyakula vyenye lishe ikiwemo mboga na matunda ili kuongeza damu mwilini," alisema.

Aidha, alisema damu ni miundombinu ya uhai wa binadamu akiwamo mama mjamzito kwa sababu hupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua hivyo panahitajika kuwa na damu nyingi mwilini.

"Ili damu iwapo mwilini ni lazima kula chakula bora chenye lishe imara ambacho kitasaidia kuokoa maisha ya mama na mtoto," alisema.

Alisema miongoni mwa sababu zinazochangia ongozeko la vifo vya mama vitokanavyo na uzazi ni upungufu wa damu mwilini, sindingizo la damu na kifafa cha mimba.

Daktari huyo aliwataka wajawazito kuhudhuria kliniki mapema baada ya kugundua kuwa anaujazito ili kama kuna tatizo kubainika mapema na kupatiwa tiba inayostahiki kwa wakati.

Mwandishi wa habari mwandamizi, Salum Said Salum, aliwataka waandishi wa habari waliopatiwa mafunzo hayo ya afya ya uzazi kuwa mabalozi wazuri wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu afya ya uzazi ili kupunguza vifo vinavyoweza kuepukikika vitokanavyo na uzazi.

Mratibu wa Mradi wa Afya ya Uzazi kutoka TAMWA, Zaina Abdallah Mzee, alisema TAMWA kwa kushirikiana na Shirika la WPF kutoka Marekani imeamua kutoa mafunzo ya afya ya uzazi kwa waandishi wa habari kwa sababu hayapewi kipaumbele.

Alisema mradi huo unawajengea uwezo waandishi wa habari kutoka Unguja na Pemba, jinsi ya kuripoti masuala ya afya ya uzazi ili jamii ikiwamo wasichana na wavulana kujitambua na kuwa na uwelewa wa masuala hayo.

## Serikali yajinasibu kuwawezesha wananchi kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema imeandaa mazingira mazuri ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mitaji ya uwezeshaji ili wawekeze katika maeneo ya ujasiriamali ikiwamo katika uchumi wa buluu.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, aliyasema hayo Mjini Unguja wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matumizi ya fedha za ugonjwa wa virusi vya corona zilizopatiwa wizara hiyo.

Alisema lengo la serikali kuwasaidia wananchi kuanzisha miradi ya kiuchumi ambayo itawasaidia kuendesha harakati zao za maisha ili kujikwamua na hali ya umasikini. Aidha, alisema kwamba katika kutekeleza mpango huo serikali iliwapatia mikopo nafuu kupitia fedha hizo za ahueni ya Uviko-19 ambayo haina riba kuwasaidia wananchi hao kuendesha miradi yao.

Alisema kuwa lengo ni kuona wananchi wa Zanzibar wananufaika kutumia mikopo hiyo ambayo hutolewa kwa njia za benki ili kurahisisha upatikanaji wa fedha hizo.

Aidha, aliwataka wananchi waliokopa kupitia mkopo wa fedha hizo kuanza utaratibu wa kurejesha malipo kupitia benki kulingana na hali halisi ya mapato.

Alisema ni vyema wananchi kuweka utaratibu maalumu wa kurejesha mikopo ili kutoa nafasi kwa wananchi wengine kupatiwa mikopo hiyo kutokana na kuwa zoezi hilo ni endelevu.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetoa Sh. bilioni 36.5 ili kuwapatia wananchi mikopo nafuu isiyo na riba.




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya (kushoto), akibonyeza kitufe kuzindua huduma ya WhatsApp Chatbot 'Bwana Swala' ya Kampuni ya Precision Air, jijini Dar es Salaam jana itakayomwezesha abiria kupata tiketi yake kupitia simu ya mkononi. Katikati ni Mkurugenzi wa Biashara wa Precision Air, Lilian Massawe na (kulia) ni Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hii, Patrick Mwanri. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Dk. Mwinyi: Utalii unachangia asilimia 30 pato la uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema utalii ni sekta kuu ya uchumi na maendeleo unaoingiza asilimia 30 ya pato la uchumi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na ujumbe wa watu saba kutoka Kampuni ya Ujenzi wa Reli na Uwekezaji ya China.

Ujumbe huo ulifika kumtembelea Dk. Mwinyi pamoja na mambo mengine walikaribishwa kuangalia fursa mbalimbali za maendeleo zilizomo nchini.

Dk. Mwinyi alisema sekta tatu muhimu za uchumi wa Zanzibar ikiwamo utalii, uvuvi na kumbi za mikutano, hivyo aliwataka kuangalia namna ya kuwekeza kwenye maeneo hayo ili kutoa ushirikiano kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar na Wazanzibari kwa ujumla.

Kuhusu utalii, Dk. Mwinyi aliwaeleza wawekezaji hao kwamba Zanzibar ni kisiwa cha utalii chenye vivutio vingi vya ufukwe wa bahari na hifadhi ya kimataifa ya Mji Mkongwe.

Hivyo, aliikaribisha Kampuni ya Ujenzi wa Reli na Uwekezaji kutoka China, kuangalia fursa ya Mji Mkongwe wenye majengo ya historia kwa kufanya uwekezaji wa hoteli za kisasa ili kuwavutia Wachina wengi kuingia Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Aidha, aliwataka kuangalia namna ya kuwekeza kwenye kumbi za mikutano ya kimataifa na Zanzibar ina maeneo mengi ya mapumziko ya watalii na uwekezaji sambamba na kuwakaribisha kwenye uwekezaji wa visiwa vidogo ambavyo ni vivutio vizuri kwa watalii ili kutoa fursa kwa mataifa mbalimbali duniani kuja kuitembelea Zanzibar.

Kuhusu uvuvi, Dk. Mwinyi aliwaeleza wageni hao kwamba uvuvi ni sekta kiongiozi inayosadifu dhana nzima ya uchumi wa buluu kutokana na maumbile ya visiwa vya Unguja na Pemba kuzungukwa na Bahari ya Hindi.

Hivyo, aliwataka kuangalia zaidi uwekezaji wa uvuvi wa kina kirefu cha maji na Zanzibar ina rasilimali ya samaki wengi watakaosafirishwa hadi mataifa mengine duniani.

Pia aliwaeleza kuangalia namna ya kufanya kilimo cha samaki hai ambacho mazingira ya Zanzibar yanatuhusu ustawi wa kilimo hicho.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Meneja mwendeshaji wa kampuni hiyo, Hao Ping Dong alimweleza Dk. Mwinyi, kampuni yao ina miradi mingi ya mandeleo na tayari imewekeza maeneo mengi duniani.

Alisema sekta ya ujenzi ni sekta kuu inayojishughulisha zaidi kwenye kampuni yao pia wamejikita kwenye ujenzi wa viwanja vya ndege, hoteli na majengo makubwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

CARNIVORES SAFARIS LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T 814 BAD – TOYOTA LANDCRUSER. Chassis namba JTELB71J807080061. Engine namba IHZ0606102. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/251056/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

WILLIAM HILLARY RIWA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA TOYOTA RAV4 YENYE NAMBA ZA USAJILI T 314 BAK. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI. KAH/TR /RB/498/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA BOMA**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI/NDOA NA.07/2023**
**JINA LA MDAI: SARANEEMA RAYMOND**
**JINA LA MDAIWA: FAIDA MBOGO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa FAIDA MBOGO**
**MWANZA**
**Kwa kuwa mdai ameleta Madai yake Eleza hapa habari za Madai: MADAI YA TALAKA**

Kwahiyo unatakiwa kuja kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 03 Mwezi 08 Mwaka 2023 saa asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwakuwa siku siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili nilazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO:kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 07 mwaka 2023.
Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 07 mwaka 2023

..............................................
**HAKIMU**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**D4N COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA ZA **ROLLER** ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T 754 DMN** YENYE TAARIFA YA POLISI **KAH/ TR/RB /504 NA ROLLER** YENYE NAMBA YA USAJILI **T 674 DKD.**, TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/505/2023** PAMOJA NA KADI ZA GARI AINA YA **TIPER** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 208 DLV.** YENYE TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB 510/2023** NA GARI AINA YA HORSE YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 997DMS** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/508/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**D4N COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA ZA **TIPER** ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T 552 DLV** YENYE TAARIFA YA POLISI **KAH/ TR/RB /506** NA GARI AINA YA TIPER YENYE NAMBA YA USAJILI **T604 DLV,** TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/507/2023.** PAMOJA NA KADI ZA GARI AINA YA TIPER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 388 DML .** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/509/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA BOMA**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NA.38/2023**
**JINA LA MDAI: JUMA ABDUL TEMBO**
**JINA LA MDAIWA: BAHATI KASEKE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa BAHATI KASEKE**
**0656991305-DAR ES SALAAM (ILALA-BUNGONI)**
**Kwa kuwa mdai ameleta Madai yake Eleza hapa habari za Madai: MADAI YA TSH.2300000/=**

Kwahiyo unatakiwa kuja kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 01 Mwezi 08 Mwaka 2023 saa asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili nilazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21 mwezi 07 mwaka 2023.
**Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 07 mwaka 2023**

..............................................
**HAKIMU**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**D4N COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA ZA TIPER ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T 552 DMN** YENYE TAARIFA YA POLISI **KAH/ TR/RB /506/2023NA** GARI AINA YA TIPER YENYE NAMBA YA USAJILI **T604 DLV,** TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/507/2023.** PAMOJA NA KADI ZA GARI AINA YA TIPER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 388 DML .** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/509/2023**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Ruto akubali kukutana na Odinga

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya William Ruto, amesema yuko tayari kukutana ana kwa ana kufanya mazungumzo na kiongozi wa upinzani Raila Odinga wakati wowote.

Hatua hiyo inakuja baada ya miezi kadhaa ya maandamano ya kuipinga serikali ambayo yamezua taharuki ndani ya nchi hiyo.

Kupitia ukurasa wake wa Twiter, Ruto aliandika kwamba anakwenda Tanzania kuhudhuria mkutano wa kimataifa wa raslimali watu, akirejea yupo tayari kukutana naye kwa ajili ya mazungumzo.

"Kama unavyojua siku zote ninapatikana pale unakokujua pa kukutana na wewe ana kwa ana kwa urahisi", ilisema twitter hiyo.

Awali, Odinga aliwaambia waandishi wa habari wa kimataifa kuwa Rais wa Tanzania Samia Suluhu aliwapatanisha ili kurejesha hali ya utulivu, lakini Rais Ruto hakujitokeza kushiriki mazungumzo hayo wiki mbili zilizopita.

Odinga alisitisha maandamano mwezi Aprili na Mei baada ya Ruto kukubali mazungumzo, lakini mazungumzo hayo yalivunjika.

Hata hivyo,Muungano wa Azimio uliandaa tena maandamano mwezi huu, yaliyosababisha ghasia na Vifo vya watu zaidi ya 30.

Awali, kiongozi wa upinzani, Raila Odinga alifanya ziara hospitali kwa ajili ya kuwajulia hali watu waliojeruhiwa na polisi wakati wa maandamano.

Odinga baada ya kutoka hospitalini hapo alielekea katika mkesha wa kuwaombea watu waliouawa katika maandamano ya kupinga kupanda kwa gharama ya maisha.

**BBC**


# TANGAZO

## VIWANJA VINAUZWA KIGAMBONI NA MOROGORO

**KINGSWAY PARK CO LTD WANAUZA VIWANJA VILIVYOPIMWA MAENEO YAFUATAYO:**

1. KIBADA KIGAMBONI KARIBU SHANGWE SHOPPING KILOMITA 1.5 TOKA MAIN ROAD 30,000 KWA SQUARE METER
2. DEGEKARIBU NA MRADI WA NSSF BEI YAKE 15,000 KWA SQUARE METER.
3. KIHONDA MOROGORO MANISPAA KARIBU NA STATION YA SGR BEI YAKE NI 15,000 KWA SQUARE METER.
4. KIWANJA CHA SHULE SQUARE METRE 75,681 SAWA NA EKARI 18.7 KIPO KINGULUWILA MOROGORO.

BEI YAKE NI 4,500 KWA SQUARE METER.

**KWA MAWASILIANO PIGA NAMBA**
**+255 655 100 644 AU +255 787 228 900**
**+255 656 967 444**


# Meli iliyobeba magari 3,000 yawaka moto

**AMELAND, Uholanzi**

MELI iliyobeba magari 3,000 inateketea kwa moto katika bahari ya pwani ya kisiwa cha Ameland nchini Uholanzi.

Moto huo umesababisha kifo cha baharia mmoja na wafanyakazi wengine 22 wamejeruhiwa.

Operesheni kubwa ya uokoaji inaendelea kwa kutumia vyombo mbalimbali katika eneo la Bahari ya Kaskazini ambayo imeorodheshwa kuwa eneo la Urithi wa Dunia.

Wafanyakazi 22 walipelekwa hospitalini wakiwa na matatizo ya kupumua na kupata majeraha ya kungua,

Msemaji wa walinzi wa pwani ya Uholanzi, alisema kuwa moto huo huenda ulisababishwa na moja ya magari 25 ya umeme yaliyokuwa kwenye meli hiyo.

Picha zilizochukuliwa na walinzi wa Pwani zilionyesha Meli hiyo yenye bendera ya Panama ikiwa inafuka moshi mzito.

Mmoja wa walinzi katika pwani hiyo aliambia shirika la habari la Uholanzi (ANP) kuwa moto huo unaweza kuendelea kuwaka kwa siku kadhaa.

Meli hiyo ya mizigo iliondoka katika bandari ya Bremerhaven kaskazini mwa Ujerumani mwendo wa saa 9:00 kwa saa za huko siku ya Jumanne kuelekea Port Said nchini Misri.

**BBC**



Wanajeshi wa Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wakisimama pembeni ya kambi zilizoteketezwa na moto na waasi wa Codeco hivi karibuni. **PICHA: DW**


Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

## MABORESHO KWENYE MIFUMO YA KIBENKI

**Ndugu Mteja,**

Benki ya TCB inatarajia kufanya maboresho kwenye mifumo yake ya kibenki kwa muda wa siku mbili mfululizo kuanzia siku ya Ijumaa tarehe 04 Agosti 2023 saa sita usiku hadi Jumapili 06 Agosti 2023 saa tano asubuhi. Hivyo wakati wa zoezi hilo matawi yetu yote yatafungwa pamoja na kukosekana kwa huduma nyingine kama POPOTE Mobile, ATMs, Internet Banking na WAKALA ndani ya muda tajwa katika siku zilizopangwa.

Kutokana na zoezi hilo benki inawashauri wateja wetu kufanya miamala nje ya muda wa maboresho ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza kutokana na maboresho hayo.

Maboresho haya muhimu yanalenga kuongeza ufanisi kwenye mifumo ili kuwahudumia wateja wetu kwa ufanisi Zaidi.

Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza na tunatanguliza shukrani zetu za dhati kwa ushirikiano wenu.

**Imetolewa na Kitengo cha:**
**Uhusiano na Mawasiliano**
**Simu: 0762 283836**


# Ujumbe wa Russia, China wawasili Korea Kaskazini

**PYONG YANG, Korea Kaskazini**

UJUMBE wa Russia ukiongozwa na Waziri wa Ulinzi Sergei Shoigu, umewasili nchini Korea Kaskazini, kwa ajili ziara ya kiserikali.

Hata hivyo, viongozi hao watajumuika na ujumbe kutoka China, katika sherehe za kumbukumbu ya miaka 70 ya kumalizika kwa Vita vya Korea, vinavyoadhimishwa kwa kufanyika gwaride la kijeshi.

Ziara hizo ni za kwanza za aina yake kuelekea Korea Kaskazini tangu ilipofunga mipaka yake ili kujaribu kudhibiti janga la Covid 19.

Haijulikani ikiwa hii inaashiria mabadiliko katika sera za mipaka ya nchi hiyo.

Korea Kaskazini ilijitenga na uhusiano wote wa kibiashara na kidiplomasia mwanzoni mwa 2020, hata kwa nchi za Russia na China, ambazo ni washirika wake wakuu wa kiuchumi na kisiasa.

Korea Kaskazini imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa chakula, ambao unatokana na kufungwa kwa mipaka yake na vikwazo vikali vya kimataifa ambavyo vimewekwa kwa sababu ya mpango wake wa nyuklia. **BBC**

# KARIA: CECAFA U-18 YAANZA MAANDALIZI KOMBE LA DUNIA

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

RAIS wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Wallace Karia amesema mashindano yanayoendelea hapa nchini ya wasichana chini ya miaka 18 yanayoandaliwa na Baraza hilo ni sehemu ya maandalizi ya timu hizo ikiwemo Tanzania kujiandaa na mashindano ya kombe la Dunia la wasichana.

Akizungumza na Nipashe juzi katika ufunguzi wa mashindano hayo yanayoendelea kwenye dimba la Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, Karia ambaye pia ni Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) alisema Tanzania walikubali kuwa wenyeji wa mashindano hayo ili kuyanusuru na kufanya timu za ukanda huu zitakazoshiriki mashindano ya Dunia kuweza kupata michezo ya maandalizi.

Alisema awali mashindano hayo yalitakiwa kufanyika nchini Kenya lakini yalishindikana na kuamua kuyaamishia Tanzania ambapo hata hivyo Kenya wameshindwa kushiriki kwa sababu ya wachezaji wao wengi wako mashuleni.

"Tumeamua kuokoa mashindano haya ambayo maandalizi yake awali yalisuasua, tuliona itakuwa vyema yakifanyika kwa muda ili timu za taifa kupata matayarisho ya kujipanga na mashindano mbalimbali ikiwemo WAFCON, Olympic na mashindano ya kombe la Dunia kwa wasichana wenye umri wa chini ya miaka 20," alisema Karia.

Kuhusiana na mashindano hayo yanayoendelea katika Uwanja wa Azam Complex, Karia amewaomba Watanzania kujitokeza kushuhudia michezo hiyo ambayo timu zimeonyesha ushindani mkubwa.

"Mashindano yameanza vizuri tunaona wachezaji wanaonyesha ushindani mkubwa sana na naamini makocha wamepata kipimo kizuri cha matayarisho ya timu zao," alisema Rais huyo wa CECAFA.

Katika mashindano hayo Tanzania ilianza vizuri kwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Burundi katika mchezo wao wa kwanza na mchezo unaofuata watacheza na Ethiopia leo.

# Tabora United wajivunia kumpata Kopunovic

**Na Saada Akida**

BAADA ya Uongozi wa Tabora United (zamani Kitayosce FC) kufanikiwa kumpata kocha wa zamani wa klabu ya Simba, Goran Kopunovic umeweka wazi kuwa wana imani na kocha huyo na wana uhakika wa kuonyesha ushindani mkubwa kwenye msimu mpya wa 2023/24.

Tabora United ni miongoni mwa timu tatu zilizopanda daraja kucheza ligi kuu msimu ujao zingine zikiwa JKT Tanzania na Mashujaa FC kutoka Kigoma.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa timu hiyo, Rashid Hassan alisema wanaimani na kocha huyo kufanikisha malengo yao ya kuwa timu itakayoonyesha ushindani mkubwa kwenye Ligi.

"Tumemchukuwa Goran kwa sababu tunafahamu uwezo wake aliwahi kupita hata Tanzania na usajili tunaofanya nina imani kubwa tutafikia malengo yetu ya kuwa timu yenye ushindani mkubwa kwa wapinzani wetu tutakaokutana nao kwenye msimu huu wa ligi," alisema Rashid.

Kwa upande wake kocha Goran alisema anafurahi kurejea Tanzania kwa mara nyingine na kuifundisha Tabora United ambayo anaamini wataonyesha ushindani mkubwa katika ligi.

Alisema anaimani kubwa na usajili wa timu yake na wanaendela na maandalizi ya msimu mpya wa ligi kwa kuhakikisha wanaenda kuonyesha ushindani mkubwa kwa wapinzani wao.

"Nimefurahi sana kurejea Tanzania, tuko katika maandalizi mazuri tunaendelea kujiandaa tukiwa nyumbani Tabora, bado nina uzoefu na ligi ya hapa na nimeona wachezaji wako vizuri tutafika malengo yanayotarajiwa na Watu wa hapa," alisema Kocha huyo.

Bodi ya Ligi Kuu (TPLB) imetangaza msimu mpya wa ligi hiyo 2023/2024 utaanza Agosti 15.




Kiungo wa Simba, Clatous Chama akiwa amevaa 'gloves 'kwenye mazoezi ya gym nchini Uturuki muda mfupi baada ya kumalizika kwa mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake. **PICHA: BIN ZUBERY**

## JKT Tanzania yaitaka nafasi ya 4 Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa klabu ya JKT Tanzania umesema malengo yao ni kushika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023,2024 unaotarajiwa kuanza Agosti 15 mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana,Mwenyekiti wa timu hiyo Kapteni Godwin Ekingo alisema wamefanya maboresho kwenye maeneo ambayo wamebaini yalikuwa na mapungufu ili kuipa nguvu timu yao kuelekea msimu ujao.

"Tumefanya maboresho kwenye maeneo ambayo tulibaini mapungufu kwa kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani ndani ya kikosi chetu msimu ujao na kuifanya timu kufanya vizuri na kufikia malengo yetu ya angalau kushika nafasi ya nne mwisho wa msimu," alisema Kapteni Ekingo.

Aidha, alisema mpaka sasa tayari wamemaliza kufanya usajili na watatoa taarifa ya tarehe ambayo watatangaza wachezaji wao wapya pamoja na walioachana nao kupitia siku yao ya 'Usiku wa JKT'.

## Mapambano Muay Thai kufanyika kesho Dar

**Na Abdallah Maraka**

KAMPUNI ya Bongo Boxing Fighting (BFC) imeandaa mapambano 14 ya ngumi aina ya Muay Thai (Ngumi za Thai) yatakayofanyika keshokutwa Jumamosi katika ukumbi wa Superdom Masaki, Jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Masoko wa Startimes Media, David Malisa alisema wameshirikiana na BFC kuendeleza mchezo huo na mingine ijayo ikiwemo kickboxing ili kuendelea kuinua vipaji vya wachezaji wa mchezo huo.

"Wengi walitamani kuona mchezo wa Muay Thai, niwaambie wakae mkao wa kula, Jumamosi ijayo tutawaletea mapambano hayo"alisema Malissa. Kwa upande wake muandaaji wa pambano hilo Scott Patrick alisema kutakuwa na pambano kuu litakalomshirikisha bondia Abdul Ubaya dhidi ya bondia kutoka Uganda Ivan Mgumba watakaowania Mkanda wa Dunia wa WBC.

Aidha Patrick aliwataja mabondia wengine watakaopanda ulingoni katika mapambano ya utanguluzi ni pamoja na Emanuel Shija dhidi ya Yusuph Fundi, Mbaraka Mtange dhidi ya Paul Owen, Abdulrazaki Kazumari dhidi ya Emanuel Patrick, Mwingereza Tomiwa Akindele dhidi ya Johnson Kihegula, Imani Matendo dhidi ya Frank Epimaki.

Aidha, wengine watakaopambana ni Musa Said atakayepigana na Mkenya Amos Lion, Scott Farrel dhidi ya Marcus Warry, Fariche Joseph dhidi ya Mzimbabwe, Chiedza Homakoma na Hamis Msondo dhidi ya Ajemi Amani.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANE ANUKIA BAYERN

UHAKIKA wa Bayern Munich wa kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane kutoka Tottenham Hotspur unazidi kuongezeka na hawajali kuhusu taarifa za kwamba Paris St-Germain pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. **(Sky Sports)**

### BAYERN YAKOMAA

MTENDAJI wa Mkuu wa Bayern Munich, Jan-Christian Dreesen na Mkurugenzi wa ufundi, Marco Neppe wamebaki Ujerumani, badala ya kujiunga na timu kwenye kambi ya huko Japani, ili kukamilisha mpango wa pauni milioni 100 kwa ajili ya kumsajili Harry Kane. **(Mirror)**

### MBAPPE AGOMBEWA KILA KONA

KLABU ya PSG inatarajia kupokea ofa ya fedha pamoja na mchezaji kutoka Klabu za Ulaya ili kumuuza Kylian Mbappe, baada ya kupokea ofa ya rekodi ya dunia ya pauni milioni 259 kutoka kwa Al-Hilal. Chelsea, Manchester United, Tottenham, Inter Milan na Barcelona zimeonyesha nia ya kumuhitaji mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. **(Press Association, via Independent)**

### SUZUKI AIKATAA MAN U

GOLIKIPA wa Urawa Red Diamonds na Japan Zion Suzuki mwenye umri wa miaka 20 amekataa kuhamia Manchester United. **(Sponichi)**

### BERNARDO SILVA HAUZWI

KLABU ya Manchester City imemwambia kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva kuwa haina nia ya kumuuza msimu huu wa joto licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kutaka kuondoka. **(90dk)**

### MAGUIRE AWANIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imefanya mazungumzo ya awali na Manchester United kuhusu kumsajili beki wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30 na kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 26. **(Sky Sports)**

### ...WAMWINDA PIA GALLAGHER

OMBI la West Ham la kumnunua kiungo wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, limekataliwa lakini wana imani kuwa wanaweza kuipiku Tottenham kupata saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England. **(Standard)**

### LAVIA KUBAKISHWA

KLABU ya Southampton imekataa ofa inayodhaniwa kuwa ya thamani ya pauni milioni 35 kutoka Liverpool kwa ajili ya kiungo wa kati raia wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka19, huku klabu hiyo ya Pwani ya Kusini ikitaka angalau pauni milioni 50. **(Guardian)**

### FABINHO HAONDOKI LIVER

UHAMISHO wa kiungo wa kati wa Liverpool na Brazil, Fabinho kwenda Al-Ittihad ya Saudi Arabia uko hatarini kuvunjika huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 akitarajiwa kuanza tena maandalizi ya msimu mpya akiwa na wekundu hao wa Anfield. **(The Athletic)**

### KIMMICH KUBAKI

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich anatarajiwa kubakia Bayern Munich baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kusema kwamba, hana uhakika wa kupata muda mwingi wa kucheza kwenye kikosi cha kwanza cha klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, katika msimu unaokuja. **(Sky Germany)**

### DARLOW ATAKIWA LEEDS

LEEDS United ianataka kumwongeza kipa, Karl Darlow kwenye kikosi chao na wanaonekana kupiga hatua katika jitihada zao za kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kutoka Newcastle United. **(The Athletic)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LIONEL MESSI AZIDI KUNG'ARA MAREKANI

●●●Afunga mabao mawili na kuasisti mengine kwenye mchezo wake wa kwanza akiwa na timu yake mpya ya...

**FLORIDA, Marekani**

LIONEL Messi alifunga mabao mawili na kutoa asisti katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Atlanta United wakati yeye na Sergio Busquets walipokuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Inter Miami CF Jumanne usiku kwenye Uwanja wa DRV PNK mjini Fort Lauderdale, Florida, kwa mara ya kwanza tangu ajiunge na timu hiyo ya Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Haikuchukua muda kwa wachezaji hao wa zamani wa Barcelona kufanya vyema, huku Busquets akiinua mpira mzuri juu ya safu ya ulinzi ya Atlanta kwa Messi, ambaye alikosa jaribio lake la kwanza, lakini akafunga kwa mpira uliorudi na kuifanya Miami kuongoza kwa 1-0 katika dakika ya nane.

Messi aliongeza bao lingine katika shambulizi la dakika ya 22 na akatoa pasi kwa Robert Taylor, aliyefunga bao la tatu kwa Miami na kuipa timu hiyo faida ya 3-0 wakati wa mapumziko ya mechi ya Kombe la Ligi.

Taylor alifunga bao nne kwa Miami baada ya mapumziko kwa pasi ya Messi, ambaye alitolewa dakika ya 78 huku akishangiliwa sana na mashabiki.

Busquets alitolewa zikiwa zimesalia dakika sita na nafasi yake kuchukuliwa na Victor Ulloa.

"Ilikuwa mchezo mzuri na nimefurahi tuliweza kuwafurahisha mashabiki wetu. Mchezo mzuri sana na tulichukua hatua nyingine katika mwelekeo sahihi," alisema kocha wa Miam, Gerardo Martino baada ya mchezo huo.

Miami ilisonga mbele hadi hatua ya 32 katika Kombe la Ligi. Atlanta imekuwa klabu ya 100 ambayo Messi amefunga dhidi yake.

Busquets na Messi walitumia miaka 13 kucheza pamoja katika kikosi cha kwanza cha Barcelona kabla ya Muargentina huyo kuhamia Paris Saint-Germain mwaka 2021, na wameendelea kuwa marafiki wa karibu tangu mbio zao za kubeba kombe kule Camp Nou.

"Miaka mingi tukicheza pamoja, kwa hiyo ni rahisi sana kucheza naye," alisema Busquets.

"Nina furaha sana kuwa karibu naye." Messi na Busquets waliingia kama wachezaji wa akiba katika mechi zao za kwanza katika ushindi mnono dhidi ya Cruz Azul siku ya Ijumaa ambao ulimfanya Messi kufunga bao kwenye mchezo huo kwa mkwaju adhabu ndogo.

Martino alimsimamia Messi na Busquets kwa msimu mmoja kule Barcelona na alisema baada ya mechi hakushangaa kuona wakicheza kwa uwelewano mzuri.

"Wachezaji hawa wawili ni wazuri sana kwa kile wanachofanya, wanatengeneza nafasi," alisema Martino alisema.

HABARI MICHEZO

# AZAM, SINGIDA FG WATAKA MAKUNDI SHIRIKISHO AFRICA

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya kuchezeshwa droo ya michuano ya kombe la Shirikisho na klabu bingwa Afrika, klabu za Azam na Singida Fountain Gate zimesema zinataka kufika angalau hatua ya makundi.

Azam na Singida Fountain Gate zitaiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika na tayari zimeshajua wapinzani wao wa awali kwenye michuano hiyo.

Azam wataanzia ugenini kucheza na Bahir City Kenema ya Ethiopia wakati Singida Fopuntain Gate wataikaribisha JKU ya Zanzibar kwenye michezo ya hatua ya awali ya michuano hiyo.

Endapo timu hizo zitashinda kwenye michezo hiyo ya hatua ya awali itakayochezwa kati ya Agosti 18-20, Azam watakutana na Club Africans ya Tunisia na Singida itakutana na Future Club ya Misri.

Kocha wa Azam FC, Youssouph Dabo amesema baada ya kupangwa droo wengi wanaamini mechi yao ya kwanza dhidi ya Bahir ni nyepesi lakini ukweli sivyo hivyo na kwamba hawezi kuifikiria mechi dhidi ya Club Africain kabla ya kumalizana na Bahir Dar Kenema.

"Tunatakiwa kwenda stepu kwa stepu, hakuna haja ya kuanza kuifikiria Club Africain kabla ya kumalizana na Waethiopia, tunatakiwa kuanzia sasa akili yetu na mawazo yaelekee katika mechi ya kwanza, tunatakiwa kuwaheshimu wapinzani wetu wote ambao tutakutana nao, tukianza kuwafikiria Watunisia zaidi na kuwadharau tunaoanza nao basi tunakuwa tumejiweka kwenye hatari," alisema kocha huyo akiwa nchini Tunisia ambako kikosi cha timu hiyo kimeweka kambi ya maandalizi ya msimu ujao.

Hata hivyo, amesema lengo lao kama klabu kushinda hatua kwa hatua hadi kufikia makundi ambako wataangalia upepo unakwendaje kwenye ngazi hiyo.

Kwa upande wake, Ofisa habari wa timu hiyo, Hasheem Ibwe amesema msimu huu wamedhamiria kufanya vyema ingawa hawezi kusema kwamba watakwenda robo fainali, nusu au fainali, ila lengo ni kutinga hatua ya makundi.

"Nikiri kuwa misimu miwili iliyopita hatukuwa vizuri, msimu uliopita tulitolewa na Al Akdar ya Algeria, lakini safari hii tumedhamiria kuwa na nyakati nzuri, tukiwaambia mashabiki wetu kama tunakwenda robo fainali, nusu au fainali yenywe itakuwa ni kuwapaka mafuta kwa mgongo wa chupa, tumeweka malengo kuwa tunatamani kucheza hatua ya makundi," alisema Ibwe.



Kiungo wa Timu ya Taifa ya wasichana wenye umri chini ya miaka 18, Joyce Fred (kulia), akiwania mpira na mshambuliaji wa Burundi, Estella Gakima kwenye mchezo wa michuano ya Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) juzi, Tanzania ilishinda mabao 3-0. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Mkandala, Ng'ondya watua Kagera Sugar ikiacha saba

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI aliyepewa 'thank you' na Azam FC, Cleophace Mkandala ametua kwenye klabu ya Kagera Sugar, akitia kandarasi ya miaka miwili, huku ikiacha jumla ya wachezaji saba.

Klabu hiyo pia imepata saini ya mchezaji wa Mbeya City, Richardson Ng'ondya kuitumikia kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Kagera Sugar imeanza kukisuka kikosi chake baada ya kutofanya vema msimu uliomalizika, ikimaliza ligi na pointi 35, ikishika nafasi ya 11, lakini pia ilikuwa moja ya timu ambazo hazikuwa na uhakika wa kubaki na ilikuwa na hatihati ya kucheza mechi za 'play off' hadi ligi ilipomalizika.

Mkandala alimaliza mkataba wake na Azam ambayo ilimsajili kutoka Dodoma Jiji misimu miwili iliyopita, ilikiipiga kumbo Simba kumuwania mchezaji hiyo.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo inasema usajili wa wachezaji hao ni kwa ajili ya kukitengeneza kikosi hicho ili kiwe cha kutisha kuelekea msimu ujao wa ligi.

Taarifa hiyo ilisema bado inaendelea na mchakato usajili huku ikiwa imeacha baadhi ya wachezaji ambao hawawahitaji tena kuendelea nao.

Wachezaji waliopewa 'thank you' na Kagera Sugar ni Jackson Kibirige, Laurent Alfred, Yusuph Mhilu, Abeid Athumani na Yusuph Dunia. Erick Mwijage, Meshack Mwamita.

## Yanga yapania kuvuka kikwazo cha miaka 24

INATOKA UK. 24

"Mwalimu yupo na ratiba yake akishirikiana na jopo lake kutengeneza utimamu wa mwili wa wachezaji wetu, lakini pia anaanza kupenyeza mbinu zake za kiufundi, wachezaji wanafanya mazoezi mara mbili asubuhi na jioni kuna wakati asubuhi wanakuwa gym jioni uwanjani, wakati mwingine wanabadilisha mazoezi, haya ni mambo ya kiufundi na nadhani pia baada ya ratiba walimu wataanza kuwafuatilia wapinzani tutakaokutana nao," alisema Kamwe.

## Robertinho: Simba ni kubwa haiogopi timu yoyote Afrika

INATOKA UK. 24

tana nayo na wapo tayari kukutana na timu yoyote Afrika.

Alisema walipofikia sasa timu nyingine za Afrika zinahofia kukutana nayo kwenye michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya vilabu Afrika.

"Tunajiamini, tunaamini kiwango chetu, Simba ni levo nyingine kabisa kwa sasa, tena safari hii ina kikosi kipana sana, tuna timu imara na yenye nguvu, tuna benchi la ufundi lililo bora, tunawaheshimu wapinzani wetu wote wawili ambao mmoja wapo tutacheza naye, lakini kwa mimi nawaza mbele zaidi siyo hapa, ukifikiria makubwa utakuwa mkubwa tu, Simba inacheza kwa kiwango cha juu sasa na itafika mbali," alisema Robertinho.

Alisema walipofikia sasa timu nyingi za Afrika zinahofia zaidi kukutana nayo kutokana na rekodi yao nzuri katika miaka ya karibuni.

Simba ambayo haitoanzia mechi za awali, itaanza kampeni yake ugenini, Septemba 15 itakapocheza na mshindi kati ya timu hizo zitakazocheza pambano la awali la kwanza nchini Namibia, Agosti 18 kabla ya kurudiana Agosti 25 nchini Zambia.

Robertinho aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kwenye wiki ya Simba Day ili kuona ambacho benchi lao la ufundi imekifanya kwenye 'pre season.' yao kwenye jiji la Ankara.

"Ni muhimu sana kuwaheshimu pia mashabiki wetu, tukipata sapoti kutoka kwa mashabiki kuanzia kilele cha Simba Day itakuwa siku nzuri sana kwa nchi, unajua Watanzania wanapenda sana soka kama ilivyo Brazil, itakuwa ni siku nzuri ya kuwaona vijana wao, wachezaji wa zamani na wapya, mipango yetu, mifumo ya kucheza soka, benchi la ufundi pamoja na kiwango kizuri tutakachoonyesha siku hiyo," alisema.

Simba itacheza dhidi ya Power Dynamos ya Zambia kwenye kilele cha Wiki ya Simba Day, Agosti 6, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Iwapo timu hiyo ya Zambia itaitoa African Stars, Simba na Power Dynamos zitakutana mara tatu msimu huu, moja ikiwa ni Simba Day na mara mbili kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema mashabiki wa timu wategemee mambo mazuri kwenye tamasha lao kabla ya kuanza mzimu mpya wa Ligi Kuu.

# Michezo

Alhamisi Julai 27, 2023


Nipashe




**Lionel Messi azidi kung'ara Marekani** UKURASA 21

# Robertinho: Simba kubwa, haiogopi timu yoyote Afrika

●●●Asema ilipofikia sasa timu pinzani ndizo zinazoogopa kukutana nao, wapo tayari...



**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho', amesema kwa sasa klabu hiyo si hiyo inayoogopa kukutana na timu pinzani bali wapinzani wao ndio wanaoogopa kukutana na Simba kutokana na ubora wao.

Kauli hiyo ya Robertinho imekuja siku moja baada ya Shirikisho Soka Afrika (CAF) kupanga droo ya michuano ya klabu bingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Katika droo hiyo Simba imepangwa kuanzia raundi ya pili kuwani kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ikisubiri mshindi wa mchezo utakaowakutanisha Africans Stars ya Namibia dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

Akizungumza kutoka Uturuki walipoweka kambi kujiandaa na msimu mpya, Robertinho alisema hakuna timu wanayoihofia kuku-

UKURASA. 23



# YANGA YAPANIA KUVUKA KIKWAZO CHA MIAKA 24

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema akili yao ya safari hii imejielekeza kumaliza msimu unaowasumbua wa kushindwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa miaka 24 sasa.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo Ali Kamwe amesema jana kuwa baada ya ratiba ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka juzi, malengo yao kwanza yanafikiria kuvunja mwiko huo ambao umekuwa ukiwasumbua tangu mwaka 1998 ilipotinga mara ya kwanza na ya mwisho hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga imepangwa kucheza dhidi ya AS Ali Sabieh Telecom (ASAS) ya Djibouti Agosti 18 ugenini, na marudio yake yatakuwa mwezi huo huo, tarehe 25, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Kubwa ambalo la kuwaambia wanachama na mashabiki wa Yanga malengo yetu makubwa ni kufika kwanza hatua ya makundi, tumeweka malengo ambayo yana uhalisia ndani yake, hatutaki kutengeneza presha yoyote kwa wanachama, mashabiki wetu na benchi la ufundi, kwa muda mrefu timu yetu haijacheza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa hiyo ni lazima tuanze kwa kufika hapo kwanza na hapo unafikaje? Ni lazima ushinde mechi ya awali halafu uende kwenye hatua inayofuatia," alisema Kamwe.

Akizungumzia wapinzani wao, Kamwe alisema ingawa ni wageni masikioni mwa mashabiki wa soka hasa wa Tanzania, lakini imekuwa ni timu ya mafanikio nchini mwao, hivyo amewaonya mashabiki kutoibeza na kuokena kama Yanga tayari imeshasonga mbele.

"Si timu kongwe kama Yanga kwenye soka, lakini si ngeni kwenye ramani ya soka, ni ngeni tu kwenye masikio ya watu wengi wa soka hasa hapa nchini lakini imekuwa ina mafanikio kwenye soka la Djibouti, imechukua mataji ya pale na ina wachezaji pia kutoka nje ya nchi wanaocheza soka la kulipwa hapo, kwa sasa viongozi ni lazima tuanze kuangalia ni jinsi gani tutacheza nayo, mazingira ya uwanja tutakaoenda kucheza, nchi yenyewe, hoteli za kule zipoje na viwanja vya mazoezi, niwaambe tu wanachama na mashabiki kuwa wasidanganyane, Ligi ya Mabingwa kuna timu ngumu, tusianze kuwaza mchezo unaofuatia wakati wa kwanza bado," alionya Kamwe.

Iwapo Yanga itasonga mbele kwenye hatua ya raundi ya kwanza itakutana na mshindi kati ya Al Merrikh ya Sudan na AS Otoho d'Oyo ya Congo Brazavvile kuwania kutinmga hatua ya makundi.

Akizungumzia maandalizi alisema Kocha Mkuu, Miguel Gamondi amekuwa akishirikiana na makocha wa utimamu wa mwili kuwaweka wachezaji wao sawa na huku akipenyeza mbinu zake za kiufundi.

UKURASA. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >